# Nipashe

Jumamosi Desemba 12, 2020 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580427

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper LIKE & FOLLOW US




**Majangili** 12,000, silaha za kivita zanaswa hifadhini

UKURASA 3



**Shahidi** aeleza Mawazo kuteswa hadi kifo chake

UKURASA 4

**Naweza kumbakiza Messi Barcelona - Font**

A 22

# Magufuli ampa kibarua Naibu Waziri Madini

• **Amtaka** kusafisha uovu uliopo, aagiza waliokuwa TMAA kukatwa mishahara... *Endelea ukurasa 2*



## YALIYOMO

UKURASA WA 4

**SERIKALI SASA YAJIPANGA UDHIBITI UTOROSHAJI MADINI**

KUTOKANA na wimbi la utoroshaji madini, serikali wilayani Chunya mkoani Mbeya, imetangaza mikakati mipya...

## Maalim Seif, Dk. Shein wasalimiana tangu 2015

UKURASA 10



Makamu wa Kwanza wa Rais Zanzibar, Maalim Seif Sharif Hamad, akisalimiana na Rais mstaafu wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, walipokutana katika dua maalum ya kuiombea nchi amani, katika Masjid Mushawarra, mjini Unguja, juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store



## Salma atumia historia ya uchumba na Kikwete kuwafunda wasichana

UK. 3

MICHEZO YANGA: MWADUI HAWACHOMOKI UK.24 MAONI, KATUNI UK.6

# Aagiza waliokuwa TMAA wafyekwe mishahara

**Na Romana Mallya**

RAIS John Magufuli ameagiza waliokuwa watumishi wa Wakala wa Ukaguzi wa Madini Tanzania (TMAA) na kuhamishiwa Tume ya Madini Tanzania, kupunguziwa mishahara yao.

Amemwagiza Katibu Mkuu Kiongozi, Balozi John Kijazi kushirikiana na Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Dk. Laurean Ndumbaro, kuhakikisha wanasimamia utekelezaji huo mara moja.

Rais Magufuli alitoa agizo hilo, jana, Ikulu ya Chamwino, Dodoma wakati wa hafla ya kumwapisha Prof. Shukrani Manya kuwa Naibu Waziri wa Madini.

Akizungumza baada ya kumwapisha, Rais Magufuli alisema ameamua kuweka wazi uamuzi huo, ili wahusika hao wafahamu kwamba mishahara yao inapunguzwa na kwamba asiyekubaliana na uamuzi huo aache kazi.

Rais Magufuli aliwataka watumishi hao katika utekelezaji wa kupunguza mishahara yao wasitafute mchawi, ndiyo sababu ameamua kuliweka wazi suala hilo.

Alisema watumishi hao walipokuwa awali (TMAA) walikuwa na mishahara mizuri, lakini serikali ilifuta wakala huo kwa sababu walishindwa kufanya kazi.

"Mlihamishwa TMAA mkaja huku (Tume ya Madini) na mishahara yenu. Katibu Mkuu Kiongozi hiyo mishahara ipunguzwe kwa sababu walitakiwa wapunguzwe kazi. Kazi waliyoifanya TMAA ilikuwa ya ovyo ila hatukutaka kuhukumu jumla," alisema.

"Kwa hiyo haiwezekani upelekwe Tume ya Madini, ulitoka na mshahara wa Sh. milioni 10 unamzidi hata mkurugenzi wako, unamzidi hata Mwenyekiti Mtendaji, bosi wako anapokea mshahara wa Sh. milioni tano wewe Sh. milioni 10," aliongeza.

Rais Magufuli alisema watumishi hao hawawezi kuwa na mishahara mikubwa inayowazidi mabosi hao, kwamba anayetakiwa kuzidiwa mshahara ni yeye (Rais) ambaye anapokea Sh. milioni tisa, huku Kamishna wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) akipokea Sh. milioni 15.

"Tume ya Madini lazima tupitie kanuni, mtu akifanya vizuri anapandishwa kidogo, hawa waliokuja ambao hawakufanya kazi vizuri wanateremshwa, ila kama wapo ambao hawataki kuteremshwa waache kazi, watafute kazi nyingine," alisema Rais Magufuli.

"Huu ndio ujumbe wangu, Katibu Mkuu Kiongozi ulitakiwa hili uwe umelifanya mapema kwa hiyo ukashirikiane na kumpa maagizo Katibu Mkuu Utumishi. lazima watu hao waanze kushushwa mishahara," alisisitiza.

Rais Magufuli alisema suala la kushusha mishahara watumishi wa serikali halijaanzia hapo, kwamba walikuwapo wakurugenzi ambao walikuwa wakijilipa mishahara hadi Sh. milioni 25.

"Nilitegemea wataacha, lakini wote wameendelea kufanya kazi. Ninataka tutende haki ili tusitengeneze makundi ya watu wanaofanya kazi vizuri halafu walioboronga mahali fulani wanakuja na kuendelea na mishahara hiyo," alisema Rais Magufuli.

Aidha, Rais Magufuli aliagiza endapo kuna sheria au kanuni ya aina hiyo ni lazima ibadilishwe.

"Watu wote wanahitaji mishahara mizuri, ninajua mmenielewa, waziri mshirikiane nao, ninapenda wanaofanya kazi vizuri wapate mishahara mizuri, lakini wanaofanya vibaya ninataka wakose kabisa au wapate kidogo sana ili liwe fundisho kwao kujifunza kufanya kazi," alisema na kuongeza:

"TMAA walipata fedha mno, ninajua huu ujumbe umeeleweka na ninajua wengine mpo hapa mlikuwa TMAA, mjue mishahara inakwenda kupungua, ila kama unashindwa acha kazi, ili ukafanye kazi nyingine."



Rais Dk. John Magufuli akimwapisha Prof. Shukrani Manya kuwa Naibu Waziri wa Madini, katika viwanja vya Ikulu ya Chamwino, mkoani Dodoma jana. **PICHA: IKULU**

# JPM ampa kibarua Naibu Waziri Madini

**Na Romana Mallya**

RAIS John Magufuli jana, alimwapisha Prof. Shukrani Manya kuwa Naibu Waziri wa Wizara ya Madini, huku akimpa maagizo mazito ambayo anapaswa kwenda kuyashughulikia.

Prof. Manya aliapishwa baada ya aliyepaswa kushika nafasi hiyo, Francis Ndulane, kushindwa kuapa mbele ya Rais Magufuli juzi.

Akizungumza baada ya kumwapisha Ikulu ya Chamwino, Rais Magufuli alimtaka Prof. Manya kuhakikisha anatumia taaluma yake kuinua sekta ya madini, ili ichagize zaidi kwenye pato la taifa.

Prof. Manya ni mtaalamu wa masuala ya madini na kabla ya hapo alikuwa Mtendaji Mkuu Tume ya Madini Tanzania.

"Akiba haukuwa wewe tu, bado tuna wengine, wachezaji mliochaguliwa pamoja na wewe mkachape kazi, maagizo mmeshapewa hapa na mengine ya kwenye ilani," alisisitiza.

**SABABU KUMTEUA**

Rais Magufuli alieleza kuwa alimchagua Prof. Manya kwa sababu ndani ya wizara hiyo hususani nafasi za juu inaonyesha kuyumba kiutendaji kwa sababu haina watu wenye taaluma hiyo.

"Waziri wa Madini hajui madini taaluma yake ni mwalimu, Katibu Mkuu amesomea masuala ya kompyuta hayana uhusiano na Copper (shaba), uranium, tumeona tukuweke wewe ukawe kiunganishi, wewe ni Profesa haina maana maprofesa waliowahi kukaa Wizara ya Madini walifanya vizuri," alisema na kuongeza:

"Uende na mtazamo huo. Tumewahi kuwa na Waziri wa Madini profesa, Katibu Mkuu profesa tena wa madini, lakini mambo hayakwenda vizuri. Ninataka nikuhoji kwenye mtego huo ambao maprofesa wenzako waliufanya walipokuwa Wizara ya Madini," alisema na kuongeza kuwa amelazimika kumweleza ukweli kwa sababu hataki kumficha.

"Ninajua umefurahi, umeshangilia na watu wako wa Tume ya Madini wameshangilia ninajua walikuwa wanakwamishwa na baadhi ya mambo, nenda ukayatatue."

"Pili, sekta ya madini ni muhimu, mkijipanga vizuri, mkahusishe wataalamu, mkienda na ushirikiano mzuri ambao tumeanza kuona ishara nzuri za mapato katika wizara hii, kwa sababu wakati wanaingia kina Biteko (Waziri wa Madini) makusanyo yalikuwa Sh. bilioni 168, makusanyo ya mwaka huu ni Sh. bilioni 527," aliongeza.

Rais Magufuli aliwataka wataalamu katika sekta hiyo kujiuliza ni kwa nini Tanzania ina kila aina ya madini yakiwamo ya chuma, lakini hayachimbwi na kuyeyushwa na kutengenezewa chuma, badala yake yanatumika mataruma ya reli yanayoibiwa. "Haya ndiyo maswali magumu ambayo mnatakiwa kuyafanya, yale mliyosoma kwa nadharia mkayatekeleze kwa vitendo, pameshindikana kitu gani, wenye viwanda wanaotengeneza nondo na chuma," alisema.

"Mkawafundishe, waanze kuyeyusha vyuma. Inawezekana yasiwe na viwango vyote, lakini wakafanye hata kama ni kumpa bure na faida ni nyingi zipo ikiwamo ajira kwa vijana, madereva na mapato kwa serikali yatapatikana," alisisitiza.

Aidha, Rais Magufuli alihoji kwa nini madini ya graphite yanayopatikana nchini hayajaanza kuchimbwa hadi sasa, kwamba yanamsubiri nani wakati wataalamu wa madini wapo. Vilevile, Rais Magufuli alihoji kwa nini madini ya makaa ya mawe (coal) yasitumike kama nishati mbadala na kuagiza uongozi wa Wizara ya Madini kujipanga na kufanya kazi usiku na mchana kuhakikisha makaa ya mawe yaliyopo nchini yanaanza kutumika.

"Viwanda vya saruji vinalalamika havipati coal (makaa ya mawe) ya kutosha. Tumesikia kiwanda cha Mtwara cha Dangote, akienda kule anapimiwa, nimeambiwa kuna mtu amehodhi sifahamu kama ameshaondoka ama bado yupo," alisema Rais Magufuli na kuongeza:

"Kwa nini hii Coal ya Tanzania isitumike kama nishati mbadala wakati wataalamu wapo, kwa nini isitumike kutengeneza nishati, ni jukumu la Wizara ya Madini kujipanga vizuri mkafanya kazi usiku na mchana ili ukombozi na zawadi tuliyopewa na Mungu yaanze kutumika."

Kadhalika, Rais Magufuli alihoji kwa nini nchi kama Uganda wameanza kutengeneza kwa kutumia Uranium yao lakini Tanzania bado. "Lazima tufike mahali tuchangamkie zawadi tulizopewa na Mungu katika kujenga uchumi wa nchi, ninakupongeza na kukupa pole kwa sababu wapo maprofesa wenzako waliofeli," alisema na kuongeza:

"Na wewe nitakuwa nakuangalia kwa jicho, nilijiuliza nichukue tena profesa ambaye aliwahi kuzungumza yaliyopo kwenye mchanga ni asilimia 0.002 na walipofanya uchambuzi wakakuta kuna asilimia nyingi." Rais Magufuli alisema anaamini Naibu Waziri huyo (Prof. Manya) atatumia taaluma yake katika kulinda ukweli.

"Nimekusikiliza wakati unaapa umesema unamshukuru Mungu amekuchagua tena siku ya mwisho, ambapo sabato inaanza kesho (leo), kaitumie sabato vizuri kwa ajili ya kufanya kazi ya Mungu, watu watakukumbuka," alisema.

## HABARI KITAIFA



Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Ardhi, Prof. Evaristo Liwa (wa pili kushoto), akitoa zawadi kwa mwanafunzi bora wa jumla Jasumine Mndeme, katika hafla iliyofanyika chuoni hapo, jijini Dar es Salaam jana. Kushoto ni Naibu Makamu Mkuu wa Chuo Taaluma, Prof. Gabriel Kassenga. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Majangili 12,000, silaha kivita zanaswa hifadhini

**Alisema kuna uwezekano wa kutumia njia ya kung'oa ila mizizi hubaki na kuota tena, huku njia ya kuchoma ikohofia kusambaza mbegu zaidi, na kwamba Hifadhi ya Taifa ya Arusha kuna miiba mikubwa imeota kwa mingi ni tishio kwa uoto wa asili.**

**Na Salome Kitomari, DODOMA**

MAJANGILI 11,838 wamekamatwa katika hifadhi mbalimbali za taifa kwa kipindi cha miaka minne kuanzia 2015/16 hadi 2018/19, huku silaha zilizohusika katika matukio hayo, zikiwamo za kivita, zikikamatwa pia.

Akiwasilisha mada ya umuhimu wa mfumo wa kijeshi katika shughuli za uhifadhi jijini Dododma jana, wakati wa mkutano wa wahariri na waandishi wa habari waandamizi wa habari za uhifadhi na utalii katika hifadhi za taifa, Kamishna Msaidizi Uhifadhi na Utekelezaji Sheria, John Nyamhanga, alisema silaha na majangili hao walikamatwa katika operesheni zilizofanywa na Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA).

Alisema kutokana na matumizi ya silaha za kijeshi na teknolojia ya kisasa kunakofanywa na majangili, lilianzishwa jeshi la uhifadhi chini ya kaulimbiu ya 'Ujasiri na Uzalendo; ambalo limefanikiwa kwa kiasi kikubwa kukabiliana na ujangili.

Nyamhanga alisema mwaka 2016/17 majangili walikuwa 115 walishuka hadi 54 na mwaka huu walikamatwa 10 na kwamba idadi hiyo ni ndogo, lakini madhara ni makubwa kutokana na ujangili unaotumia teknolojia.

Pia alisema kuanzishwa kwa Jeshi la Uhifadhi kumesaidia kuimarisha uhifadhi, lakini kuna changamoto za ujangili wa wanyamapori, misitu, uwapo wa silaha za kivita, kiraia zilinazotumika kwenye uhalifu kwenye ujangili na kasi ya uingizwaji wa mifugo hifadhini.

Aliitaja changamoto nyingine kuwa ni kuongezeka migogoro kati ya binadamu na wanyamapori kiasi cha wanyama kukosa mwelekeo na mabadiliko ya tabia nchi ambayo huleta ukame na magonjwa ya mlipuko.

Nyamhanga alisema tatizo kubwa ni wahalifu kutumia maeneo ya hifadhi kama maficho kuhatarisha usalama wa nchi huku akitolea maeneo ya Udzungwa, Hifadhi ya Mto Ngara ambako kuna kikundi cha kijamii kiitwacho Sanjo ambacho kilikuwa kinafanya mazoezi hifadhini na silaha za kivita na wanapambana na askari ikiwamo kusimamisha magari na kupora.

Alisema kukundi hicho kilitaka kujitengenezea himaya yake kwa kutumia maeneo yaliyohifadhiwa, na kutokana na faida ya jeshi la uhifadhi alikisambaratisha.

"Hifadhi za siku nyingi ziko hatarini kama Serengeti, Katavi, Arusha, Tarangire, Manyara, Mkomanzi, Kilimanjaro, Udzungwa, Saadani, huku hifadhi tano zikiwa salama ambazo ni Gombe, Mahale, Rubondo, Kitulo, Ibanda, Burigi Chato, Rumanyika na Saanane," alibainisha.

**MIMEA TISHIO**

Awali, akiwasilisha mada ya Uhifadhi na Ushirikishwaji Jamii, Kamishna Msaidizi Godwell Meing'ataki, alisema kuna tishio kubwa la mimea vamizi kwenye hifadhi za taifa ambayo kwa sasa ni zipo aina 69 na kwamba isiposhughulikiwa inaua mimea ya asili, chakula kinachotegemewa na wanyama na wakati mwingine husambazwa kwa kinyesi cha wanyama na kusambaa kwenda hifadhi na maeneo yaliyohifadhiwa.

Alisema kuna uwezekano wa kutumia njia ya kung'oa ila mizizi hubaki na kuota tena, huku njia ya kuchoma ikohofia kusambaza mbegu zaidi, na kwamba Hifadhi ya Taifa ya Arusha kuna miiba mikubwa imeota kwa mingi ni tishio kwa uoto wa asili.

Aidha, alisema uwepo wa barabara inayopita hifadhini umechangia mimea vamizi kwa kuwa watu wanatupa machungwa, mtikiti, matunda mengine yenye mbegu mbegu ambayo huota.

**UJIRANI MWEMA**

Meing'ataki alisema TANAPA inachangia asilimia 70 ya huduma za kijamii na jamii asilimia 30 ya nguvu kazi, ila kumekuwa na changamoto kwa jamii kutoa fedha na ndipo waliongeza mchango ulifika asilimia 90 na jamii asilimia 10 kwa kazi ndogo ndogo.

Alisema hadi mwaka huu miradi 451 yenye thamani ya Sh. bilioni 16.5 ya shule, nyumba za walimu, samani na zahanati.

# Salma atumia historia ya uchumba na Kikwete kuwafunda wasichana

**Na Romana Mallya**

MKE wa Rais mstaafu wa Awamu ya Nne, Jakaya Kikwete, Mama Salma Kikwete, ametumia historia ya maisha yake na mumewe kuwafunda wasichana kutambua thamani yao ndani ya jamii.

Akizungumza katika kongamano la wasichana, jijini Dar es Salaam, Mama Salma alifunguka kuwa neno la kwanza alilotamkiwa na Kikwete siku ya kwanza walipokutana, akimwambia anataka amuoe lakini ilichukua muda kutoa majibu.

Mama Salma aliwaeleza vijana kuwa msichana ni chombo chenye thamani.

"Nilisoma Nachingwea wakati huo nikiwa chuo, mume wangu Dk. Jakaya Kikwete aliniona, nikifika hatua hii naguswa sana, nimesoma chuo cha ualimu Nachingwea miaka miwili.

"Sikuijua nyumba aliyokuwa akiishi Katibu wa CCM (Chama Cha Mapinduzi) Wilaya (Kikwete) kwa sababu nilijua thamani yangu. Nilimaliza masomo nikaenda JKT Ruvu (Jeshi la Kujenga Taifa) kwa mujibu wa sheria. Kabla ya kwenda Ruvu siku hiyo nilikuwa nakwenda Posta, tulikuwa na sheria kali ukitoka chuo hakuna nyumba yoyote unaruhusiwa kuingia," alisema.

Mama Salma alisema siku moja Kikwete alimwita ofisi kwake na baada ya salamu alimuuliza kama amepata ujumbe wake.

"Nikamwambia nimeupata. Hii sijawahi kumwambia mtu yoyote, neno la kwanza aliponitamkia tulipokutana ana kwa ana, aliniambia angependa anioe. Baada ya kauli hiyo nilitoka nje, nilikuwa na rafiki yangu tukaenda kununua embe kisha tukaenda chuoni," alisema.

Mama Salma alisema baada ya kutoka kwenye ofisi ile, alipata wasiwasi kwa sababu wanachuo hawatakiwi kuingia nyumba yoyote.

"Ila haukuwa wasiwasi sana kwa sababu alikuwa amekuja chuoni kwetu. Mpaka ninamaliza chuo alikuwa anafuatilia kwa dada aliyekuwa anamtuma kwangu ambaye sikumpa jibu la ndiyo au hapana. Majibu ya ndiyo au siyo ilikuwa mpaka nimemaliza JKT Ruvu.

"Ndiyo maana katika video ya mume wangu akitimiza miaka 50, waandishi walimuuliza huyu mama ulimpata vipi, akajibu kuwa nilimsumbua," alisema.

Mama Salma aliwaeleza wasichana kuwa si kweli wanaume wanapowaambia hawalali wanawawaza kuwa ni kweli.

"Tena anasema usingizi sipati, hivi kama haupati anakuotaje. Wasichana ni lazima tujitambue, tujithmini, tujue utu wetu na thamani yetu. Siyo yule anayekwambia leo ninakupenda atakuwa mwenza wa maisha yako, anakupotezea muda na kukuondolea thamani yako," alisema.

Aliwaeleza kuwa msichana ni lulu hivyo wajitunze kwa sababu ikiondolewa haiji tena.

# Serikali yajipanga udhibiti wa madini

**Na Thobias Mwanakatwe**

KUTOKANA na wimbi la utoroshaji madini, serikali wilayani Chunya mkoani Mbeya, imetangaza mikakati mipya ya kukabiliana na tatizo hilo kwa kujenga kituo cha polisi katika kata ya Kambikatoto. Hatua hiyo inatokana na kata hiyo kutumiwa na wahalifu kama uchochoro wa kufanikisha uhalifu wao.

Mkuu wa Wilaya ya Chunya, Simon Mayeka, akizungumza na gazeti hili jana kwa njia ya simu, alisema ujenzi wa kituo hicho katika kata hiyo ambayo ni ya mwisho kabla ya kuingia mikoa ya Tabora na Singida, utaanza rasmi Januari, mwakani na kitasaidia pia kuthibiti utoroshaji mazao ya misitu. Mayeka alisema wameamua kujenga kituo cha polisi katika kata hiyo baada ya kubaini kuwa wahalifu wengi wamekuwa wakitumia kata ya Kambikatoto kutorosha madini, hivyo kusababisha serikali kukosa mapato yake.

"Tulikuwa na kituo cha polisi kimoja tu eneo la Lupa Tingatinga ambacho ukishakipita hicho unaingia mkoa mwingine. Wahalifu wanapitia kata ya Kambikatoto ambako ukitoka makao makuu ya wilaya ni kama kilometa 250 na kutoka kituo cha polisi cha mwisho ni zaidi ya kilometa 150. Kwa hiyo unaweza kuona hili eneo lilichangia udhaifu fulani," alisema. Mayeka alisema mkakati mwingine walioweka wa kukabiliana na utoroshaji wa madini ni kuongeza vizuizi na kufanya mabadiliko ya mara kwa mara kwa watu wanaokuwa katika vizuizi hivyo kwa kuwa wahalifu wamekuwa wakicheza na udhaifu wa baadhi ya watu wanaokuwapo kwenye maeneo hayo.

Mayeka alisema wilayani ina kikosi kazi kwa ajili ya kushughulia masuala hayo lakini ni bahati mbaya baadhi wamekuwa si waaminifu kwa kuvujisha siri na kuwafikia wahalifu na wao kubadilisha mbinu. Desemba 9, mwaka huu, wakati akiwaapisha mawaziri na naibu mawaziri, Rais John Magufuli alisema bado vitendo vya utoroshaji wa madini katika Wilaya ya Chunya vinaendelea na kumwagiza Waziri wa Madini, Doto Biteko, kushughulia suala hilo.

Kutokana na agizo hilo, Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP), juzi iliidhinisha wafunguliwe mashtaka sita askari polisi wawili ambao walipewa rushwa ya Sh. milioni 150 na wafanyabiashara wa madini ili kufanikisha utoroshaji wa dhahabu wilayani Chunya. Wengine watakaokumbana na mashtaka hayo ni wafanyabiashara watatu ambao wanadaiwa kuwa wamiliki wa madini hayo ambayo thamani yake haijatajwa yaliyokuwa yakitoroshwa. Mkurugenzi wa Mashtaka, Biswalo Mganga, katika taarifa yake, aliwataja watuhumiwa ambao wameshafunguliwa mashtaka kuwa ni Koplo Hassan Njujilo na Konstebo Daniel Mrema.

Wafanyabiashara watakaoungana na askari hao ni Sabra Habib Ally, Malof Salum Nassor na Hamdun Stamily Mtafuni.

Mganga alisema mashtaka watakayokumbana nayo ni utakatishaji wa fedha haramu kinyume na sheria ya kuzuia utakasishaji fedha haramu sura 423 marejeo 2019, kujihusisha na uhalifu wa kupangwa kinyume cha Sheria ya Kuzuia Makosa ya Uhujumu sura 200 marejeo 2019 na kupokea rushwa kinyume cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa sura 329 marejeo 2019.

Mashtaka mengine yatakayowakabili ni kutoa rushwa kinyume cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, matumizi mabaya ya nafasi kinyume cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa sura 329 ikisomwa pamoja na Sheria ya Kuzuia Makosa ya Uhujumu Uchumi na Uhalifu wa Kupanga na Usafirishaji Madini bila kibali kinyume kwa karibu na mchimbaji mdogo wa madini Hamdun Stamily Mtafuni.



Wachuuzi wa ndizi wakisubiri wateja katika soko la kuu la Mabibo, jijini Dar es Salaam jana. Mkungu mmoja wa ndizi unauzwa kwa bei ya 25,000/- hadi 27,000/- kulingana na aina ya ndizi. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Shahidi aeleza Mawazo alivyokamatwa na watuhumiwa na kuteswa hadi kufa

**Na Joctan Ngelly** GEITA

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Geita imeendelea kusikiliza kesi ya mauaji ya mgombea ubunge Jimbo la Busanda, Alphonce Mawazo kupitia Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) inayowakabili washtakiwa watano wanaosadikiwa kuwa wafuasi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Washtakiwa hao ni Alfan Apolinari (41), Epafra Zacharia (39), Hashim Sharif (45), Habibu Feruzi (34) na Kululinda Bwire (31) wote kwa pamoja ni wakazi wa Katoro mkoani Geita.

Washtakiwa hao wote kwa pamoja, jana walifikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Geita majira ya saa 2 asubuhi na kupandishwa kizimbani majira ya saa 3 asubuhi mbele ya Naibu Msajili Mahakama Kuu Tanzania Kanda ya Mwanza, Frank Mahimbali.

Mahimbali ambaye ni Hakimu Mkazi Mwandamizi, alipewa mamlaka (Extended Jurisdiction) kusikiliza kesi hiyo.

Upande wa Jamhuri unaongozwa na Javelin Rugaihuruza ambaye ni Wakili wa Serikali Mkuu, Hezron Mwasimba ambaye ni Wakili wa Serikali Mwandamizi na James Pallangyo, Wakili wa Serikali.

Upande wa utetezi unaongozwa na mawakili wa kujitegemea watano ambao kila mmoja anamtetea mshtakiwa mmoja. Mawakili hao ni Yisambi Siwale, Flora Enosy, Laurent Bugoti, Abel Sizya na Paul Hombo.

Mahimbali alikubaliana na ombi hilo na kuanza kusikilizwa kwa kesi hiyo ambapo mashahidi wanne wa upande wa Jamhuri walitoa ushahidi wao. Shahidi wa tisa upande wa Jamhuri, Said Omary (25) mkazi wa Katoro, akiongozwa na Wakili Pallangyo, alidai kuwa alimpata mteja ambaye alikuwa anakwenda Nyumba ya Kulala Wageni ya Mbalu na nauli ilikuwa Sh. 1,000 kutoka Panama kwenda huko.

Alidai kuwa mbele aliona magari mawili aina ya Toyota Landcruiser yakiwa yamewasha taa na yakiwa na mwendo wa kasi kuonyesha kama kuna hatari.

"Mimi nilimuuliza abiria wangu Mawazo mbona yanakuja kwa kasi, Mawazo akaniambia hakuna wewe ongeza spidi. Badaye akasema ongeza spidi watakuwa wananifuatilia, ndipo mimi nikaongeza spidi hadi hapo anapokwenda.

"Nilipofika Mbalu Gesti gari moja lilinipita na kusimama mbele ya yangu likani- 'block' (likanizuia) na lingine nyuma yangu, mimi nikawa katikati. Baada ya kuniziba mbele na nyuma watu walishuka na kumvuta Mawazo ambaye alikuwa abiria wangu ambaye alikuwa amekaa kwenye pikipiki yangu na mimi nikakimbia na kuacha pale pikipiki yangu, alidai.

Shahidi huyo alidai kuwa watu ambao walikuwa wakimpiga Mawazo, aliwatambua na wengine walikuwapo jana, mahakamani hapo na baadhi hawakuwapo.

Aidha, aliwataja washtakiwa ambao walikuwa wakimshambulia Mawazo kuwa ni Alfan Apolinary ambaye alikuwa anampiga Mawazo kwa fimbo miguuni, shingoni na mgongoni na alikuwa amevaa nguo za kawaida, Epafra Zacharia, alikuwa na silaha ya aina ya moko inayotumika kuchimbia dhahabu na alikuwa anampiga Mawazo kichwani na kisogoni.

Omary aliwataja wengine kuwa ni Hashim Sharif aliyekuwa na fimbo alikuwa anampiga Mawazo kichwani na kwenye mabega, Habibu Feruzi aliyekuwa akimpiga mateke miguuni na Kululinda Bwire alikuwa na rungu akawa anampiga Mawazo miguuni na kichwani.

Baada ya Wakili Pallangyo kumaliza kumwongoza shahidi wa upande wa Jamhuri, upande wa utetezi ukiongozwa na mawakili wake, walimuuliza maswali shahidi huyo kama ifuatavyo;-

**Wakili:** Wewe ndiye uliyetoa taarifa kukamatwa kwa mshtakiwa Kululinda Bwire?

**Shahidi**: Ndiyo.

**Wakili:** Wakati gani unaongea ukweli na wakati gani unaongea uongo?

**Shahidi:** Wakati huu ndiyo naongea ukweli.

**Wakili:** Washtakiwa walikuwa wanampiga Mawazo kwa zamu?

**Shahidi:** Walikuwa wanamshambulia wote kwa pamoja.

Baada ya mawakili wa kujitegemea kumaliza kuuliza maswali shahidi, upande wa Jamhuri ukiongozwa na Rugaihuruza uliendelea kumuuliza maswali shahidi kama ifuatavyo.

**Wakili:** Taarifa ya kwanza kabisa kutoa kituo cha polisi maelezo yako ni tarehe ngapi?

**Shahidi:** Siku ya kwanza kabisa ni Novemba 16, mwaka huu ndiyo, nilienda kutoa maelezo yangu polisi.

**Wakili:** Wakati unaanza kuendesha pikipiki ulikuwa na miaka mingapi?

**Shahidi:** Nilikuwa na miaka 18.

Katika kesi hiyo ya mauaji tangu ianze kusikilizwa mashahidi tisa wameshatoa ushahidi wao na vielelezo sita kwa upande wa Jamhuri. Upande wa Jamhuri unatarajia kupeleka zaidi ya mashahidi 20 mahakamani na vielelezo vinane.

Baada ya hapo, Mahimbali aliahirisha kesi hiyo hadi kesho kwa ajili ya kuendelea kusikiliza mashahidi wengine waliobakia. Washtakiwa wote kwa pamoja walipelekwa mahabusu kwa sababu kesi inayo wakabili ya mauaji haina dhamana.

Akisoma hati ya mashtaka jana, Msaidizi wa Kumbukumbu Mahakama Kuu Tanzania Kanda ya Mwanza, Martina Nelei, alidai kuwa Novemba 14, 2015 katika Kijiji cha Rudete Mkoa wa Geita washtakiwa wote kwa pamoja walimuua Alphonce Mawazo kitendo ambacho ni kinyume cha kifungu 196 na 197 cha Sheria ya Kanuni ya Adhabu sura ya 16 kama ilivyofanyiwa marekebisho mwaka 2002.

HABARI KITAIFA

# Askofu Ruwa'ichi ataja mwarobaini elimu Afrika

**Na Joseph Mwendapole**

ASKOFU Mkuu wa Kanisa Katoliki Jimbo Kuu la Dar es Salaam, Jude Thaddaeus Ruwa'ichi, amesema nchi za kusini mwa Jangwa la Sahara zina chaguo moja tu la kuwezesha wananchi wake kupata elimu bora kama zinataka kuendelea na kuondokana na ujinga, umaskini na maradhi.

Aliyasema hayo jana wakati wa mahafali ya 13 ya Chuo Kikuu cha Mtakatifu Joseph Tanzania, Kibamba jijini Dar es Salaam.

Ruwa'ichi alisema amefurahi kusikia kuwa chuo hicho kinatekeleza mpango wa kuwaandaa wanafunzi kuibua miradi na hatimaye kuisajili kama kampuni na kutoa ajira kwa vijana wenzao pamoja na kuzalisha bidhaa mbalimbali kibiashara badala ya kuhangaika kutafuta ajira.

"Mpango huu ni muhimu sana na unaendana na mahitaji ya wakati huu ambapo serikali ya awamu ya tano chini ya Rais John Magufuli, inahimiza vijana kujiajiri. Wito wangu kwa menejimenti ya chuo ni kwamba uwekezaji katika mpango huu uongezwe ili wanafunzi wengi zaidi kutoka fani mbalimbali wanufaike nao," alisema.

Pia alivitaka vyuo vingine vya elimu ya juu kujifunza kuhusu mpango huo mzuri ambao alisema utaaongeza idadi ya wahitimu wenye uwezo wa kuanzisha kampuni, hivyo kutengeneza ajira kwa vijana wengi zaidi.

Askofu Mkuu Ruwa'ichi aliwataka wahitimu kutambua kwamba elimu waliyoipata chuoni hapa wanaitumia kwa manufaa ya jamii kwa weledi mkubwa, kwa utendaji bora na ufanisi katika fani zao.

Kadhalika, alisema madaktari wanategemewa sana kutakoe huduma bora kwa wananchi katika kupigana na adui maradhi.

"Ninawaasa wahandisi mkawe wabunifu na kuutumia ujuzi mlioupata kufanikisha lengo la serikali la kuifanya Tanzania iwe na uchumi unaotokana na maendeleo katika viwanda kwa kufanya kazi katika sekta rasmi au katika sekta isiyo rasmi," alisema.

Alitoa wito kwa Watanzania kutumia Chuo Kikuu cha Mtakatifu Joseph kwa kuwa ni chuo pekee kinachotoa elimu ya juu sambamba na kusisitiza nidhamu ya hali ya juu kwa wanafunzi wake pamoja na jumuiya yake yote.



Wahitimu wa Chuo Kikuu cha St. Joseph cha Kibamba, jijini Dar es Salaam, wakila kiapo cha utii wakati wa mahafali ya 13 ya chuo hicho jana, ambapo mgeni rasmi alikuwa Askofu Mkuu Jimbo Kuu la Katoliki Dar es Salaam, Yuda Thadei Ruwa'ichi (hayupo pichani). **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# RC awawashia moto madiwani uharibifu wa vyanzo vya maji

**Na Elizabeth John, NJOMBE**

MKUU wa Mkoa wa Njombe, Mhandisi Marwa Rubirya, amewataka madiwani wa Halmashauri ya Mji wa Makambako kusimamia kikamilifu shughuli za maendeleo katika kata zao na kuhakikisha vyanzo vya maji haviharibiwi.

Mhandisi Rubirya alisema hayo juzi kwenye kikao cha kwanza cha Baraza la Madiwani sambamba na kuapishwa kwa madiwani hao.

Alisema ni lazima kwenda kusimamia uhifadhi wa vyanzo vya maji kwa kuzuia kulima mabondeni ili kuhakikisha uwapo wa maji kwa kipindi kirefu.

"Katika vyanzo kule kuna uchafuzi mkubwa unaoendelea wa mazingira. Ukiachilia mbali, ukataji miti ni kulima katika vyanzo vya maji ni changamoto kubwa sana," alisema.

"Tujiulize ni kwa nini wananchi wanakimbilia kulima kwenye vyanzo vya maji? Ni kwa sababu kule mabondeni ndiko kwenye unyevunyevu, kwa hiyo eneo moja ambalo kwangu litakuwa ni ajenda ya kwanza ni hili. Maofisa kilimo naomba tulisimamie kwa karibu ni lazima turejee katika kilimo ambacho kinakubalika," alisema.

Aliongeza kuwa: "Mkoa wa Njombe kuna asili ya miinuko na miteremko na kwamba wanapaswa kulima kwa matuta au makinga maji. Ni dhahiri kwamba mvua zinaponyesha udongo wote wenye rutuba unazolewa kwenda mabondeni, unyevunyevu unakwenda mabondeni na ndiyo sababu kile kilimo cha kwenda kule mabondeni. Niombe Baraza la Madiwani kuhakikisha hili tunalizingatia kwa sababu ni maelekezo ya serikali."

Naye Ofisa kutoa Ofisi ya Rais Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Enock Mwaitebele, aliwasisitiza madiwani hao kuzingatia yale yote waliyoyaapa.

"Ukishaapa maana yake utayaishi hayo ambayo umeyaapa na si tu kuyatamka tu mdomoni. Myaishi na kuyatendea kazi. Kumbukeni wananchi wamewaamini kwa kuwapa kura nyingi kwa hiyo hakikisheni mnawatendea haki wananchi wenu," alisema Mwaitebele.

Diwani wa Viti Maalumu (CCM), Stella Mhemba, aliahidi kuwa wanakwenda kutekeleza kwa vitendo ilani ya uchaguzi na kwamba watashirikiana na wananchi kikamilifu. Mbunge wa Makambako, Deo Sanga, alimhakikishia Mkuu wa Mkoa kuwa wanakwenda kufanya mabadiliko makubwa ya kimaendeleo katika jimbo pamoja na kueleza umuhimu wa kutunza vyanzo vya maji kwa wananchi.

# DC aibua usiri vipigo wanaume

**Na Shaban Njia, KAHAMA**

MKUU wa Wilaya ya Kahama, Anamringi Macha, amesema baadhi ya wanaume wamekuwa wakifanyiwa vitendo vya ukatili na wake zao, lakini wamekuwa hawatoi taarifa.

Akizungumza katika maadhimisho ya Siku 16 za Kupinga Ukatili wa Kijinsia mjini hapa, Macha alisema kumekuwa na vitendo vya unyanyasaji dhidi ya wanaume, lakini vimekuwa haviripotiwi katika vyombo vya sheria.

Sababu kubwa ya kutotoa taarifa, kwa mujibu wa Macha, ni kuogopwa kuchekwa na jamii.

Wakati Macha akitoa siri hiyo, wanaume pia wamekumbushwa kulea watoto aliowazaa nje ya ndoa, ili kupunguza tatizo la kuishi mtaani pamoja na kukomesha ajira ambazo haziendani na umri wao.

Ofisa Ustawi wa Jamii wa Halmashauri ya Mji wa Kahama, Abrahamani Nuru, alisema wazazi kushindwa kuwalea watoto wa ndani na nje ya ndoa kumesababisha kuwapo ongezeko la watoto wa mitaani ambao hufanya kazi ambazo haziendani na umri wao.

Alisema kwa kipindi cha Januari hadi Septemba, mwaka huu, wamepokea mashauri ya ukatili wa kijinsia 1,627 na kati ya hayo yanayohusu watoto ni 721 na watu wazima wakiwamo wanawake ni 906 na asilimia kubwa ya watoto wanaofanyiwa vitendo hivyo ni wanafunzi.

Kamanda wa Polisi mkoani Shinyanga, Debora Magiligimba, alisema katika kupambana na ukatili wa kijinsia kwa watoto wadogo na kinamama, wanaendelea kutoa elimu ya ukatili wa kijinsia kwa wanafunzi wa shule za msingi na sekondari zilizoko mkoani Shinyanga.

Alisema kwa kipindi cha Juni hadi Agosti, mwaka huu, wamepokea mashauri 231 kulinganisha na mwaka jana, ambapo walipokea mashauri 151, sawa na ongezeko la mashauri 80 ambayo ni asilimia 53.

Mkurugenzi wa Shirika lisilo la Kiserikali la HUHESO Foundation, Juma Mwesigwa, alisema wamezijengea uwezo kamati za vijiji, kata na wilaya ili kusaidia kupambana na ukatili wa kijinsia.

**Ofisa Ustawi wa Jamii wa Halmashauri ya Mji wa Kahama, Abrahamani Nuru, alisema wazazi kushindwa kuwalea watoto wa ndani na nje ya ndoa kumesababisha kuwapo ongezeko la watoto wa mitaani ambao hufanya kazi ambazo haziendani na umri wao.**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Makocha Bara waachiwe uhuru usajili dirisha dogo

**WAKATI** mzunguko wa kwanza wa Ligi Kuu Tanzania Bara unaelekea ukingoni, Shirikisho la Soka Nchini (TFF), linatarajia kufungua mchakato wa dirisha dogo la usajili wa wachezaji kwa msimu wa mwaka 2020/21. Tayari TFF imeshatangaza usajili wa dirisha dogo utaanza rasmi Desemba 15, mwaka huu na utamalizika ifikapo Januari 15, mwakani.

Usajili huo utahusisha timu zote zinazoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara, Ligi Daraja la Kwanza na Ligi Daraja la Pili, ambazo hazikukamilisha idadi ya wachezaji 30 ambayo inatakiwa kwa mujibu wa kanuni na taratibu. Msingi wa kuwapo kwa dirisha dogo ni kutoa nafasi kwa klabu kuimarisha vikosi vyake na hatimaye kupata matokeo mazuri ambayo yatawapa mafanikio na yatatimiza malengo yao.

Ili mchakato huu ufanyike kwa mafanikio, ni vyema makocha wanaofundisha timu hizo kupewa uhuru wa kusajili wachezaji wapya ambao watawasaidia kulingana na mapungufu waliyoyabaini kwenye mechi zilizopita. Makocha ndio watu pekee ambao wanafahamu vyema idara zilizo imara na ambazo zina matatizo kwenye vikosi vyao na zitahitaji kuimarishwa ili kufikia malengo. Timu itakayotumia vyema dirisha dogo la usajili, hakika itakuwa imejiweka kwenye mazingira mazuri ya kufikia malengo yake, ingawa ni wazi tayari baadhi ya timu zimeshajitoa kwenye mbio za kuwania ubingwa.

Huu si wakati wa viongozi kushinikiza usajili wa wachezaji kwa matakwa binafsi, bali ni wakati wa kuwaachia makocha kurekebisha pale walipokosea au kuimarisha idara ambazo hazina makali.

Makocha wanapopewa nguvu ya kukamilisha usajili, inakuwa rahisi kwao katika kutekeleza majukumu na hata pale watakapofanya vibaya, inakuwa rahisi kuwatimua kwa sababu walipewa uhuru wa kusajili wachezaji watakaowapa matokeo chanya.

Si timu zote zinajipanga kufanya usajili kwa sababu hazikusajili vikosi imara, zipo baadhi ya timu wachezaji wao tegemeo wamepata majeraha ambayo yamewaweka au yatawaweka nje ya kikosi kwa muda mrefu na hivyo kushindwa kutoa mchango kwa timu yake.

Pia zipo klabu ambazo hazikufanya usajili unaoendana na ushindani uliopo kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara na hivyo kuambulia matokeo mabaya ambapo kama hawatajiimarisha, lolote linaweza kutokea kwa maana ya kubakia au kushuka daraja.


Nipashe inavikumbusha vilabu vyote kutumia muda wa dirisha dogo vizuri kwa sababu bado muda wa kurejesha kwenye mapambano upo na kamwe klabu haitakiwi kukata tamaa mpaka pale watakaposikia filimbi ya mwisho ya kumaliza msimu itakapoulizwa.

Wachezaji pia huu ni wakati wenu wa kuongeza juhudi, ili kujitengenezea nafasi ya kubakia kwenye kikosi chako au kupata ofa mpya ya kusajiliwa na klabu nyingine kwa ajili ya msimu ujao.

Mbali na kununuliwa na timu nyingine, huu ni wakati wa nyota wanaocheza ligi za ndani kutangaza vipaji vyao na kumshawishi Kocha Mkuu wa Timu ya Taifa (Taifa Stars), Etienne Ndayiragije kuwaita kwa ajili ya kwenda kupeperusha bendera ya nchi kwenye fainali za mashindano ya Kombe la Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN), zitakazofanyika Januari, mwakani nchini Cameroon.

Wadau wote wanaohusika katika kufanikisha mchakato wa usajili, wakumbuke ubora wa ligi zetu za hapa nchini, ndio hutoa mwangaza wa mafanikio ya timu za Taifa ambazo zinashiriki mashindano mbalimbali, hivyo kila litakaloamuliwa na viongozi, liwe linazingatia uzalendo. Tunatarajia pia kuona klabu zenye wachezaji wazuri, lakini hawapati namba kukubali kuwatoa kwa mkopo na kwenda kuendeleza vipaji vyao katika timu nyingine zinazohitaji huduma zao na kwa kufanya hivyo zitakuwa zimewapa nafasi ya kuimarika na baadaye kurejea kuwatumikia. Klabu kuwaruhusu wachezaji isiowatumia zitakuwa zimezingatia kulinda vipaji vya wachezaji hao, ambao si kwamba wameshuka viwango, lakini wameshindwa kupata namba kwa sababu ya ubora wa nyota waliokutana nao.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Chuki humchoma anayeihifadhi

Na Barnabas Maro

**"KUCHUKIANA** huondokesha fitina, bali kupendana husitiri makosa yote. Watu wenye akili huweka akiba ya maarifa, bali kichwa cha mpumbavu ni uangamivu ulio karibu. Yeye afichae chuki ana midomo ya uongo, na yeye asingiziaye ni mpumbavu." (Mithali 10: 12, 14, 18).

"Katika wingi wa maneno hapakosi kuwa na maovu, bali yeye azuiaye midomo yake hufanya akili. Midomo ya mwenye haki hulisha watu wengi, bali wapumbavu hufa kwa kuwa hawana ufahamu. Kwa mpumbavu kutenda maovu ni kama mchezo, bali mtu mwenye ufahamu ana hekima." (Mithali 10: 19, 21, 23).

'Chuki' ni hali ya kutokuwapo upendo, hali ya kuwa na roho mbaya, kuwa na kinyongo. 'Chukia' ni poteza mapenzi, kasirika; nuna. 'Chukio' ni hisia ya kuchukia; tendo la kuchukia. 'Chukizo' ni jambo linalochukiza; jambo linaloudhi, kukirihisha. 'Chukiza' ni kitendo cha kufanya jambo la kuudhi. Kitendo cha kiumbe kufika kiwango cha kutopendeza kwa wengine kutokana na matendo yake.

Ndivyo zilivyo Yanga na Simba zilizotengana kwa takribani miaka 84 sasa. Je, watu waliotengana kwa miaka yote hiyo waweza kuaminiana na kufanyiana wema wa aina yoyote?

"Chuki humchoma anayeihifadhi." Kwa kawaida chuki humsumbua anayeiweka. Twafunzwa umuhimu wa kutoiweka chuki kwa kuwa tunajidhuru wenyewe.

Bendera' ni kitambaa mahususi chenye rangi au nembo maalumu kinachotambulisha nchi, shirika, chama au jumuiya fulani; beramu. Wengi wetu hatutambui hilo. Ndio maana baadhi yetu hupeperusha bendera za nchi nyingine.

'Limbukeni' ni mtu aliyepata kitu au jambo asilokuwa na mazoea nalo au kupata kwa mara ya kwanza. Ndivyo baadhi yetu tulivyo. Matokeo yake tunashindwa kujua, si matumizi tu ya bendera yetu, bali hata thamani, umuhimu wake na namna ya kuipeperusha itakiwavyo!

Bendera yetu ya Taifa ina rangi nne: Bluu, Njano, Nyeusi, na Kijani. Rangi inayopaswa kuwa chini ni Bluu, ikimaanisha Bahari. Hata hivyo mara kadhaa baadhi ya watu huweka rangi ya Bluu juu tofauti ya maudhui na mpangilio wake!

Turudi kwenye mada (undani au kiini cha jambo linalozungumzwa au kujadiliwa, kusomeshwa au kuandikwa) yetu. Yanga na Simba ni watoto wa baba na mama mmoja ambao kwa ujumla wa wazazi wao, walizaliwa katika jiji moja liitwalo Bandari ya Salama. Pamoja na ukweli huo, timu hizo zachukiana mithili ya m-mbwa na paka ilhali ni wana wa wazazi wanaoishi nyumba moja!

Wageni huonyeshwa viti vyao kwani baadhi ya wenyeji huwa na viti vyao. Pia wageni huonyeshwa maliwatoni, bafuni n.k. hata kama watalala ugenini kwa siku moja tu.

'Kirumbizi' ni ngoma inayochezwa na wachezaji inayohusisha kupigana kwa fimbo. Pia ni ndege mkubwa anayefanana na kipwe, wa rangi ya njano mwenye midomo ya rangi ya chungwa mithili ya mnana ila mnana hana midomo ya rangi ya njano.

Ni ndege anayeaminiwa kuleta mkosi anapolia karibu na nyumba na ambaye ana rangi kichwani na nyeupe kifuani, anayelia kwa sauti mbalimbali. Pia ni sauti itokanayo na msuguano wa kidole gumba na kidole cha kati inayotolewa mtu anapoimba, anapotoa ishara fulani ya kumwita m-mbwa au kumtuliza mtoto au kuashiria kitu ama jambo; kifoli.

Ndivyo zilivyo Yanga na Simba. Hakuna moja inayotaka ingine ishinde kwa kile kisemwacho "bora tukose wote kwani wakipata wale hatutalala usingizi wala kutembea mitaani...!"

Hapa ndipo timu za nje hunufaika kwa ujinga na chuki zetu! Tangu Yanga na Simba zifarakane hakuna moja inayotaka maendeleo ya mwenzake ingawa zote zipo eneo moja liitwalo Kariakoo.

'Usalama' wao uwapi kama zahasimiane kila uchao na kuzinufaisha nchi za ughaibuni? Matokeo yake twafanywa mbumbumbu yaani tusiojua kitu, tusiotumia akili; wenye ufahamu mdogo wa mambo!

Ujinga wa kushirikiana na timu za ughaibuni zinazokuja kupambana na Simba au Yanga ulianza zamani wakati Yanga ilipopambana na Asante Kotoko ya Ghana kwenye michuano ya Klabu Bingwa ya Afrika. Wakati ule Yanga ilitoka mazoezini nchini Romania ikapitia Ghana moja kwa moja ili kupambana na Asante Kotoko na matokeo yalikuwa sare ya 1-1.

Mchezo wa marudiano hapa nchini, Asante Kotoko walitonywa (dokeza mtu jambo la siri kama taarifa tu au kumwepusha na hatari fulani) kwamba waruke ukuta kuingia uwanjani upande wa kushoto wa lango kuu na kweli walifanya hivyo. Sijui ni timu ipi ya kandanda Afrika isiyofanya mazingara!



Mafundi wa Mamlaka ya Maji Vijijini (RUWASA), Wilaya ya Musoma, mkoani Mara, wakijenga msingi wa tangi la maji litakalokuwa na uwezo wa kubeba lita 300,000 zitakazosambazwa katika vijiji vinne vya Kata ya Nyakatende wilayani humo, juzi. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# Bodi Korosho yabaini udanganyifu sokoni

**Na Stevie Chindiye,**
TUNDURU

BODI ya Korosho Tanzania imebaini kuwapo kwa tabia ya baadhi ya wakulima kupenyeza na kuuza korosho zilizo baki kwenye misimu iliyopita kwenye baadhi ya maghala na kuchafua soko la wakulima kwa wanunuzi wa zao hilo.

Mkurugenzi wa Bodi hiyo, Francis Alfred, alisema hayo wakati akiongea na wakulima wa Chama cha Msingi Ligunga (Amcos), wakati wa mnada wa nane wa kuuza korosho uliofanyika katika Kijiji cha ligunga, wilayani Tunduru, mkoani Ruvuma na kwamba utaratibu huo uliobainika kwenye maghala ya ukanda wa Mtama, Tunduru,

Masasi na maeneo mengine ambayo hakutaka kuyabainisha, unachafua soko hilo na kuwafanya wanunuzi kutotoa bei zenye wastani mzuri kwa wakulima.

Akifafanua taarifa hiyo, Alfred alisema kuwa, takribani tani 30,000 za korosho ndizo zilizo banguliwa katika kipindi cha msimu wa mwaka 2019 ikiwa ni kati ya tani 232,600 zilizozalishwa katika kipindi cha msimu huo na endapo mtindo huo utaendelea, upo uwezekano wa kuendelea kukosa soko la uhakika kutoka nje ya nchi.

"Hali hiyo inaonyesha kuwapo kwa utegemezi mkubwa wa soko kutoka nje ya nchi yetu, hivyo ili tuendelee kuwashawishi wateja wa mazao yetu, viongozi wa vyama vikuu kwa kushirikiana na wa vyama vya msingi, wanapaswa kuongeza utoaji wa elimu ya usimamizi wa ubora wa mazao yao wakati wanapoyakusanya na kuyapeleka sokoni," alisisitiza na kuongeza kuwa katika msimu huu wakulima wa Mkoa wa Pwani walikosa wanunuzi kwa wiki tatu mfululizo.

Alisema utaratibu wa kufanya usimamizi na ukaguzi wa korosho za wakulima kabla ya kupimwa, utasaidia kupatikana korosho zitakazo ingizwa sokoni kwa ubora utakao wavutia wanunuzi kutoka nje ya nchi kuja kununua malighafi kutoka Tanzania na kuwafanya wakulima kunufaika na nguvu kazi inayotokana na jasho lao kwa kupata faida na kujiletea maendeleo yao.

Akitoa taarifa katika mnada huo, Ofisa Ushirika, Wilaya ya Tunduru, George Bisani, alisema jumla ya kilo 2,143,846 ziliingizwa kwenye mnada huo ambao ulikuwa na wanunuzi 12 waliojitokeza na kuomba kununua korosho hizo ambao walioshinda kwa bei ya juu ya Sh. 2,226 na bei ya chini ilikuwa Sh. 2,175 kwa kilo moja.

Atoa taarifa ya mwendelezo wa malipo ya fedha za wakulima kwa niaba ya Meneja Mkuu wa Chama Kikuu cha Ushirika cha Wakulima wa Wilaya ya Tunduru Imani Kalembo, Yasini Masiano, alisema kuwa tayari chama hicho kimekwisha ingiza fedha za wakulima waliouza korosho kwenye mnada wa sita.

Akifunga mkutano wa mnada huo, Mwenyekiti wa Chama Kikuu cha Ushirika Wilaya ya Tunduru (TAMCU), Hashimu Mbalabala, aliwaomba wanunuzi kuangalia uwezekano wa kuongeza bei katika minada ijao ili kuwawezesha wakulima kumudu kufanya maandalizi ya mazao yao katika msimu ujao.

# Bil. 1.1/- kujenga miundombinu ya maji vijiji 4

**Na Sabato Kasika**

SHILINGI bilioni 1.1 zinatarajiwa kutumika katika ujenzi wa miundombinu ya kusambaza maji, kutoka Ziwa Victoria kwenda vijiji vinne vya Kata ya Nyakatende, wilayani Musoma mkoani Mara.

Ujenzi huo unasimamiwa na Mamlaka ya Maji Vijijini (RUWASA) na vijiji vitakavyonuifaka ni Kigera, Kakisheri, Kamguruki na Nyakatende.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Musoma, John Kayombo, alisema hayo alipokuwa akizungumza na gazeti hili na kufafanua kuwa mitambo ya kusafisha na kuvuta maji inajengwa kwenye kijiji cha Kigera.

"Shilingi bilioni 1.1 zinatarajiwa kutumika kwenye mradi huu, na pia Kijiji cha Kigera na kingine cha Kakisheri, ndivyo vitakuwa vya kwanza kupata huduma ya maji kutoka kwenye mradi huo," alisema Kayombo.

Kayombo alifafanua kuwa hatua hiyo inatokana na vijiji hivyo kuwa kwenye mwambao wa Ziwa Victoria, ambako mradi huo unaanzia na kisha vijiji vingine vya Kamguruki na Nyakatende vikifuatia.

"Baadhi ya maeneo ya Kijiji cha Kurukerege, kata ya jirani ya Nyegina, yatapata maji ya mradi huu na mengine yatapata kutoka Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Musoma (MUWASA)," alisema.

Mkurugenzi huyo alizitaja kata nyingine zitakazofaidika na maji ya MUWASA kupitia mitambo ya mamlaka hiyo iliopo Bukanga kuwa ni Etaro na Ifulifu.

Alifafanua kuwa wilaya hiyo ina vijiji 68 na miradi mbalimbali ya maji inaendelea kujengwa, ili kuhakikisha wananchi wote wanapata huduma hiyo.

Meneja wa mradi huo kutoka RUWASA, Mohamed Yamlinga, alisema miundombinu inayojengwa kwa sasa ni tangi la maji la ujazo wa lita 300,000 na ofisi ya maji.

"Miundombinu mingine ni vioski vya kuuzia maji na uchimbaji wa mitaro na utandazaji wa mabomba ya maji, na matarajio yetu ni kukamilisha mradi huu Januari mwaka ujao wa 2021," alisema Yamlinga.

Mwenyekiti wa Kigera, Magafu Katura, aliishukuru serikali kwa niaba ya wananchi, kwa kutimiza ahadi ya kusambaza majisafi na salama katika kijiji hicho na vingine vya Kata ya Nyakatende.

"Mradi huu unaanzia kijijini kwetu ambako imejengwa mitambo ya kusafisha na kuvuta maji kutoka Ziwa Victoria, hivyo kwa niaba ya wananchi wa kijiji cha Kigera, ninaishukuru serikali kwa jinsi anavyofanya kila njia kuhudumia watu wake katika maeneo mbalimbali nchini," alisema Katura.

# Wanafunzi 87 ARU watwaa tuzo za taaluma

**Na Mwandishi Wetu**

CHUO Kikuu cha Ardhi (ARU), kimewatunuku tuzo mbalimbali wanafunzi 87 waliofanya vizuri zaidi kwenye masomo yao.

Hafla ya utoaji wa tuzo hizo ilifanyika jana, chuoni hapo na mgeni rasmi alikuwa Makamu Mkuu wa chuo hicho, Profesa Evaristo Liwa.

Akizungumza kwenye hafla hiyo, Naibu Makamu wa Mkuu wa Chuo Taaluma, Profesa Gabriel Kassenga, alisema tuzo hizo zinalenga kutoa hamasa kwa wanafunzi wengine waendelee kuweka juhudi kwenye masomo yao wapate ufaulu wa juu.

Alisema sherehe hizo zimewezeshwa na wadau mbalimbali kwa miaka kadhaa kwa kujitolea ufadhili wa hali na mali kwa wanafunzi waliofuzu kupata tuzo hizo.

Aliwashukuru wafadhili hao na kuwaomba waendelee kuunga mkono jitihada za wanafunzi hao kwa kuwa zawadi hizo zinawasaidia kuongeza mitaji ya utendaji kazi kwa wanafunzi wa chuo hicho wanapomaliza chuo.

Alisema miongoni mwa zawadi zinazotolewa na wafadhili hao zimekuwa zikiongeza tija kwenye maisha ya wanafunzi kielimu na kiuchumi na kwamba kati ya 87, wasichana ni 43.

Alisema yuko mwanafunzi aliyeibuka mshindi wa jumla ambaye ni msichana kwa mwaka mwingine tena mfululizo ikizingatiwa kuwa wasichana ni asilimia 39 pekee ya wanafunzi waliopo chuoni hapo.

"Kwa niaba ya uongozi wa chuo, napenda kuwapongeza wote waliopewa tuzo na nawasihi waendelee kuweka juhudi kwenye masomo yao, ili waje kuwa mfano wa kuigwa kwa wanafunzi wenzao na jamii kwa ujumla, hongereni sana na nawatakia kila la kheri kwenye masomo yenu," alisema.

Profesa Kassenga, alisema leo kutakuwa na wahitimu 930 wa chuo hicho wa shahada mbalimbali na aliwapongeza wanafunzi kwa kufanya vizuri kitaaluma.

Alisema wanafunzi hao wamekuwa wakifanya vizuri kitaaluma na ni ishara kwamba kwenye juhudi mafanikio hupatikana na matumaini ya chuo ni kuendeleza jitihada hizo kwenye ujenzi wa taifa.

Baadhi ya washindi ni Mbonaga Siraji aliyeshinda zawadi saba, Mfuru Benson zawadi mbili, Hyera Maria tuzo mbili, Ngenge Clara, tuzo tatu.

Mhitimu bora upande wa wasichana, Cynthia Charles alisema, kujituma na kujali ratiba za masomo ndiyo siri kubwa ya mafanikio yake.

"Kusoma kwa bidii kuachana kabisa na starehe, nidhamu na usikivu ndiyo siri pekee ya mafanikio ya kitaaluma, nawaasa wanafunzi wenzangu kwamba wakizingatia haya watafika mbali kitaaluma," alisema Cynthia.




Mkuu wa Huduma ya Rejareja wa Benki ya Exim, Andrew Lyimo (katikati), akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam juzi, wakati akitangaza maboresho zaidi ya kampeni ya benki hiyo ya 'Chanja Kijanja na Exim Mastercard' inayolenga kuhamasisha wateja wa benki hiyo, kutumia kadi katika manunuzi ya mtandaoni au kufanya malipo kupitia mashine za malipo (POS). Kushoto ni Mkuu wa Idara ya Masoko na Mawasiliano wa benki hiyo, Stanley Kafu na Mkuu wa Idara ya Kidigitali na Huduma Mbadala, Silas Matoi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Maofisa uvuvi waonywa fedha za faini

**Na Waandishi Wetu**

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Mwanza, imeonya maofisa uvuvi wanaotoza wavuvi faini na kushindwa kuziwasilisha serikalini badala yake kuziweka mifukoni mwao.

Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Mwanza, Emmanuel Stenga, alisema hayo jana katika maadhimisho ya maadili na haki za binadamu yaliyofanyika jijini hapa.

Alisema tatizo la maofisa hao kuchukua fedha kutoka kwa wavuvi na kuziweka mifukoni mwao ili kujinufaisha, linazidi kuwa kubwa.

"Rushwa katika sekta ya uvuvi imekuwa tatizo kubwa, inamnyima haki mvuvi ambaye amekuwa akinunua nyavu halali, lakini anavyozidi kuzitumia matundu yanapanuka, mengine yanabaki kuwa madogo, hivyo maofisa uvuvi wanapomkamata wanapima kisha wanamtoza faini jambo ambalo ni uonevu," alisema.

Stenga alishauri serikali kukomesha tabia za watumishi hao ambao wamejiundia himaya za kudhulumu wavuvi kwa kisingizio cha kutekeleza sheria.

"Vita vya uvuvi haramu ijikite kwenye uagizaji na uuzaji wa zana haramu kuliko matumizi ya zana hizo.

Mtumishi wa umma anao wajibu wa kuzingatia sheria bila kushurutishwa," alisema Stenga.

Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, John Mongella, akizungumza katika kongamano hilo, alisema watumishi katika sekta ya uvuvi kutumia uwezo na ushawishi walionao kujenga uadilifu katika jamii.

"Maofisa uvuvi sijui kwa nini wameshindwa kuwa waadilifu ili kukemea vitendo vya rushwa, tabia na mwenendo ambao utawafanya wananchi kuwaamini na kuwaheshimu, jambo ambalo limekuwa gumu kupatikana kutokana na watu kulewa madaraka," alisema Mongella.

Wakati huo huo, wananchi wametakiwa kufichua watumishi wa umma wanaopokea rushwa ili kutoa huduma badala ya jukumu hilo kuiachia TAKUKURU.

Kamanda wa TAKUKURU wa Wilaya ya Maswa mkoani Simiyu, Petro Horombe, alitoa kauli hiyo wakati wa maadhimisho ya Siku ya Maadili na Haki za Binadamu katika viwanja vya stendi ya zamani mjini Maswa.

Alisema njia sahihi ya kuleta maendeleo nchini ni ushiriki wa kila mwananchi kuwafichua wala rushwa na kutoshiriki vitendo hivyo, huku akiwataka kutoa taarifa za vitendo vya rushwa katika ofisi za TAKUKURU kwa njia ya simu au kufika ofisini.

Aidha, aliwaomba watumishi wa umma kufanya kazi zao za kuwahudumia wananchi kwa uadilifu kwa kufuata viapo vyao vya kazi na wale ambao watakiuka na kujihusisha na vitendo hivyo watashughulikiwa kwa mujibu wa sheria.

Horombe aliwapongeza walimu, walezi na wanafunzi wa shule za msingi Binza, St Bakhita na Nyalikungu zilizoko mjini Maswa zenye klabu za wapinga rushwa.

- **Imeandaliwa na Rose Jacob, MWANZA na Happy Severine, BARIADI.**

# Wanafunzi 68 ujauzito miezi 11

**Na Happy Severine,** MASWA

WANAFUNZI 68 wa shule za msingi na sekondari katika Wilaya ya Maswa mkoani Simiyu wamepata ujauzito katika kipindi cha Januari hadi Novemba, mwaka huu, na kusababisha kukatisha masomo yao.

Taarifa ya Jeshi la Polisi wilayani hapa kupitia dawati la jinsia, imeeleza kuwa wanafunzi wa shule za msingi waliopata tatizo hilo ni watatu huku sekondari wakiwa 65. Idadi hiyo ilitajwa juzi na mkuu wa dawati hilo, Anande Masai, wakati wa kilele cha maadhimisho ya Siku 16 za Kupiga vita Ukatili wa Kijinsia wilayani hapo yaliyofanyika kijiji cha Shishiyu na kuratibiwa na Shirika la World Vision Tanzania. Masai alisema kesi 27 zilizohusu mimba za wanafunzi hao, zilifikishwa mahakamani, na nane kati ya hizo zimetolewa hukumu, 10 zinaendelea kusikilizwa na sita zimeondolewa mahakamani.

Alisema jamii bado imeendelea kuficha taarifa za matukio hayo ya mimba kwa wanafunzi kwa kumalizana kienyeji, ikiwa ni pamoja na kushindwa kutoa ushahidi mahakamani kwa baadhi ya kesi ambazo ziko katika chombo hicho cha haki.

Ofisa huyo alisema wamepokea matukio 148 ya ukatili wa kijinsia kwa watoto na matukio 195 kwa watu wazima wakiwamo wanaume 20 kwenye wilaya hiyo.

Akizungumza kwenye maadhimisho hayo, Mratibu wa World Vision Tanzania, Yohana Masanja, aliwataka wadau wote kuungana katika kuhakikisha vitendo hivyo vinakomeshwa kwenye jamii.

# Mbunge ataka ubunifu vyanzo vya mapato

**Na Julieth Mkireri,** BAGAMOYO

MBUNGE wa Bagamoyo, Muharami Mkenge, amewataka wataalamu wa halmashauri kubuni vyanzo vipya vya mapato vitavyoisaidia halmashauri hiyo kutekeleza mipango yake ya maendeleo iliyojiwekea.

Mkenge aliyasema hayo jana muda mfupi baada ya shughuli ya kuapisha madiwani wa Baraza la Halmashauri hiyo kukamilika.

Alisema uwapo wa vyanzo hivyo vitasaidia kuongeza makusanyo ya mapato na kufanikisha miradi mingi ya maendeleo kufanyika kwa wakati.

Mbunge huyo alisema iko baadhi ya miradi inakwama kwa kuchelewa kwa fedha za serikali endapo halmashauri hiyo itabuni vyanzo vipya vya mapato hakutakuwa na kikwazo cha maendeleo.

Katika baraza hilo, Diwani wa Viti Maalum, Ummy Matata, alitoa angalizo kwa halmashauri uwapo wa wakazi wapya wakitumia kigezo cha uwekezaji ambao wanapopatiwa ardhi kubwa hawaitumii kwa malengo husika, hivyo kukwamisha maendeleo.

Naye Apsa Kilingo alisema maendeleo katika halmashauri hiyo yanakwama kutokana na maeneo mengi kuhodhiwa na watu wachache wanaitumia kigezo cha uwekezaji, hali inayochangia maeneo mengi kuwa mapori.

Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Mohamed Usinga, aliwautaka uongozi wa afya kuboresha huduma, ambapo katika maeneo ambayo bado yana vikwazo katika utoaji wa huduma.

HABARI KITAIFA

# Simbachawene aasa watendaji kutokubali kutumika

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

WAZIRI wa Mambo ya Ndani ya Nchi, George Simbachawene, amewataka wafanyakazi wa wizara hiyo, kutokubali kutumika, wawe wavumilivu na wazalendo kwa nchi yao, ili kukuza amani na usalama.

Waziri Simbachawene alisema Jeshi la Polisi, Uhamiaji ni kiungo cha usalama wa nchi, kama hawajatekeleza wajibu wao vizuri yote yaliyofanyika yanaweza kuharibika. Aliyasema hayo jana jijini hapa wakati akifungua kikao cha Baraza la Wafanyakazi wa wizara hiyo cha kujadili taarifa ya utekelezaji wa majukumu hadi kufikia robo ya pili ya mwaka 2020/2021.

Simbachawene alisema kila moja anatakiwa kuwa mzalendo kwa kulinda amani na usalama wa nchi na wasikubali kutumika, wavae uzalendo kwa ajili ya nchi yao.

"Naomba msikubali kutumika mnatakiwa kuwa wazalendo kwa nchi yenu," alisema Simbachawene.

Alisema Baraza la Wafanyakazi si kwa ajili ya kudai haki pekee, bali ni pamoja na kutimiza wajibu wanaotakiwa kufanya.

"Daini maslahi huku mkijua mnalo jukumu la kutoa mchango wenu katika maendeleo ya taifa," alisema.

Alisema serikali tangu mwaka wa fedha 2020/2021 uanze kumekuwa na mtiririko mzuri wa fedha kutoka Hazina hali iliyosaidia watumishi kuanza kupata stahiki zao hususan malipo ya likizo na utekelezaji wa shughuli mbalimbali za wizara.

Pia, alisema vyombo vya ulinzi na usalama vilisimamia uchaguzi mkuu uliopita kwa weledi na kudhihirisha idadi ya Watanzania walivyokomaa katika demokrasia za vyama vingi na wameudhihirishia ulimwengu kwa vitendo.

Hata hivyo, alisema Rais Magufuli amekuwa akifanya kazi kubwa ikiwamo ujenzi wa miundombinu ya umeme katika Bonde la Mto Rufiji, ununuzi wa ndege na mengine.

"Haya maendeleo yanayofanyika yanahitaji mtu kuwa na roho ngumu kama Rais Dk. Magufuli ili nchi iweze kusonga mbele," alisema Simbachawe.

Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani, Khamisi Hamza Khamisi, kabla ya kumkaribisha mgeni rasmi alitaka Baraza hilo kumpa ushirikiano ili aweze kutekeleza majukumu yake kikamilifu.

"Mimi ni mgeni kwenye hii wizara naomba ushirikiano wenu ili tutekeleze majukumu ipasavyo," alisema Hamza.



Waziri wa Wizara ya Mambo ya Ndani, George Simbachawene, akizungumza wakati akifungua Baraza la Wafanyakazi wa wizara hiyo, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Pinda awaonya watumishi wa umma

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI Mkuu mstaafu, Mizengo Pinda, amesema serikali itaendelea kuwachukulia hatua watumishi wa umma wazembe na wasio waadilifu kuwatumikia wananchi.

Alisema licha ya jitihada zinazofanywa, serikali inatambua kuwa wapo watumishi wachache wamejawa ubinafsi na kujihusisha na vitendo ambavyo ni kinyume na maadili ya kazi zao.

Aliyasema hayo juzi jijini hapa, wakati akifungua kongamano la maadhimisho ya siku ya maadili na haki za binadamu kwa watumishi wa umma.

"Kila mmoja ameshamsikia Rais John Magufuli akizungumza kwa ukali na uchungu habari ya watumishi wa umma wazembe na wasio waadilifu kwamba hawana nafasi katika serikali anayoiongoza.

"Niwaase watumishi wa umma na wale walioko katika sekta binafsi kwamba wananchi ndiyo waajiri wenu hivyo kila mmoja katika nafasi yake awahudumie ipasavyo kwa weledi na nidhamu ya hali ya juu sana ili kwenda sawa na kasi ya Rais Magufuli," alisema.

Alisema serikali imefanya jitihada nyingi katika kuhakikisha kuwa utumishi wa umma unajengeka na kuwa wa kutegemewa na umma.

Alisema jitihada zilizofanyika ni pamoja na kutungwa kwa sheria za usimamizi na utendaji wa watumishi kama vile sheria ya viongozi wa maadili ya umma. "Ni matarajio yangu kuwa kongamano hili litahitimishwa kwa maazimio yenye lengo la kuboresha maeneo yote ambayo mtakubaliana kuwa yana upungufu katika uzingatiaji wa maadili mapambano dhidi ya rushwa, uwajibikaji na uzingatiaji wa haki za binadamu," alisema.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, George Mkuchika, alisema mwaka huu maadhimisho ya siku ya maadili na haki za binadamu yanafanywa kwa kongamano maalumu linalojumuisha wadau kutoka sekta binafsi na Asasi za kiraia, wabia wa maendeleo na taasisi za kidini.

Alisema lengo la maadhimisho hayo ni kuchambua masuala ya utawala bora, maadili, udhibiti wa rushwa na usimamizi wa haki za binadamu.

"Maadhimisho ya Siku ya Maadili na Haki za Binadamu hufanyika kila mwaka hapa nchini na hii imetokana na siku ya kimataifa ya kupambana na rushwa na siku ya haki za binadamu ambapo kwa mara ya kwanza ilianza kufanyika mwaka 2016," alisema Mkuchika.

# Wakulima wanawake watoa ushauri uboreshaji kilimo

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WANAWAKE ambao ni wakulima wadogo wameishauri serikali kufanya maboresho ya sera za kilimo, taratibu na mifumo ili kuwasaidia wanaojishughulisha na sekta hiyo vijijini.

Imeelezwa kuwa pamoja na kuwa na mchango mkubwa katika uchumi wa taifa, wanawake wakulima vijijini wanasumbuka na upatikanaji wa mitaji na soko lenye uhakika wa mazao yao.

Pia, kutokana na kukosa maarifa mapya wanatumia pembejeo mbalimbali bila utaratibu unaotakiwa na kusababisha hasara kubwa.

Hayo yalielezwa katika mkutano maalumu wa wakulima wadogo kutoka mikoa mbalimbali waliokuwa wakijadiliana changamoto zinazowakabili wakulima wadogo wanawake nchini na namna ya kukabiliana nazo.

Mkutano huo umeandaliwa na Jukwaa la Wakulima Wanawake Vijijini (RWFF).

Mkutano huo ambao ulifadhiliwa na Action Aid Tanzania, ulihudhuriwa pia na wawakilishi kutoka Wizara ya Kilimo na vyama mbalimbali vya kiraia.

Lengo kuu la mkutano huo kwa mujibu wa Rais wa Jukwaa hilo, Amina Senge ni kutafuta maoni ambayo yataingizwa katika mpango wa maendeleo wa sekta ya kilimo wa 2021 hadi 2026.

Alisema, wanawake wengi wanakabiliwa na matatizo lukuki katika kuendesha kilimo chao hasa upataji wa mitaji ya kuimarisha kilimo chao.

Alisema wakati umefika kwa wizara hiyo kufanyakazi karibu zaidi na wakulima wadogo wanawake kuanzia ngazi za chini ili kuimarisha tija na kuleta kipato kwa taifa.

Naye Rais wa Jukwaa la Wakulima Wanawake la Afrika, Eva Mageni, aliwataka wanawake wakulima wadogo wa Tanzania kutumia jukwaa lao kufikisha mahitaji yao serikalini.

Magreth Thomas, mmoja wa wakulima wadogo kutoka Mkoa wa Morogoro aliitaka serikali kuhakikisha kwamba inapeleka maofisa ugani vijijini kusaidia kuwapa maarifa wanayohitaji ili kukuza kilimo chao.

Alisema kwa sasa maofisa hao ni wachache na kusababisha wakulima kutopata huduma.

Mratibu wa Asasi zisizo za kiserikali wilayani Chamwino, Elizabeth Msuya, amesema ipo haja ya wadau wa kilimo kuwaangalia wakulima wenye ulemavu katika maeneo mbalimbali nchini.

Jukwaa hilo lenye wanachama 28,343 kwenye vijijini 820 ndani ya wilaya 28 nchini lilianzishwa mwaka 2017 kwa lengo la kuwapa uwezo wakulima wadogo wanawake kufahamu haki zao na kushiriki katika maamuzi makubwa ya kitaifa yanayowahusu.

# Walimu wapewa mbinu ushauri kwa wanafunzi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KATIBU Mkuu wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Dk. Idrissa Muslimu Hija, amewataka walimu kuwa wapole kwa wanafunzi katika kuwapa ushauri utakaowasaidia kuwaongoza katika maisha yao.

Akizungumza wakati akifungua mafunzo ya afya ya uzazi, jinsia na Ukimwi kwa walimu wa shule za msingi na sekondari katika ukumbi wa Kituo cha Walimu Kiembe Samaki mjini Unguja, alisema hatua hiyo itawasaidia katika kuwakinga na maradhi mbalimbali na vitendo vya udhalilishaji vinavyosababisha kupata maambukizi mapya ya virusi vya Ukimwi (VVU).

Alisema lengo la kupatiwa walimu mafunzo hayo ni kutokana na wao kuwa karibu zaidi na wanafunzi na kwamba hatua hiyo itawasaidia kuwapa ushauri kwa kutumia mbinu mbadala watakazopatiwa katika mafunzo hayo.

Dk. Idrissa alisema vijana wakati huu wa sasa wanahitaji ushauri na ukaribu zaidi kwa walimu na wazazi hasa katika masuala ya uzazi na kwamba hatua ya VVU kwa kuwaelimisha ipasavyo, ili wasijiingize katika vitendo vilivyo nje na wakati wao.

Aidha, aliwataka walimu kutojihusisha na vitendo vya udhalilishaji kwa wanafunzi kwa sababu zimeshajitokeza kesi hizo, hivyo aliwasisitiza kuwalea vizuri na kuwaona sawa na watoto wao ili wawe na maisha bora baadaye.

Pia aliwataka walimu kuyachukua mafunzo hayo na kuyatekeleza katika sehemu zao za kazi kwa vitendo na kuwatambua vizuri vijana wao kutokana na mazingira wanayoishi hivi sasa na wakati unavyokwenda ili kufikia malengo yaliyokusudiwa.

Mkurugenzi wa Mafunzo ya Ualimu, Maimuna Fadhil Abbas, aliwataka walimu kuwapa taaluma hiyo wanafunzi wao kwa usahihi ili kuwasaidia katika masuala yao mbalimbali.

Alisema mwanafunzi anatakiwa awe huru na salama wakati wote akiwa shuleni au nyumbani na wahusika wakuu wa kuwasaidia watoto kuwa salama ni mwalimu. Alisema wazazi wengi hawawaelekezi watoto wao masuala ya uzazi salama na kujamiiana pamoja na athari za maambukizi ya VVU kwa kuona aibu, hali ambayo sio sahihi.

Mafunzo hayo yameandaliwa na Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO) kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu



Mkurugenzi Mwendeshaji na Utumishi katika Wizara ya Fedha na Mipango Zanzibar, Ali Bakari Is'haka (kushoto), akiteta jambo na Mkurugenzi Mtendaji wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (ZSSF), Sabra Issa Machano, kwenye hafla ya ufunguzi wa tamasha la tatu la Zanzibar Kariakoo Festival jana. **PICHA: MARTIN KABEMBA**

# Shein, Maalim Seif wapeana mkono tangu 2015

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KWA mara ya kwanza, Makamu wa Kwanza wa Rais, Maalim Seif Sharif Hamad, na Rais mstaafu wa Zanzibar, Dk. Ali Muhamed Shein, wamesalimiana na kupeana mikono hadharani tangu kumalizika kwa uchaguzi mkuu wa mwaka 2015 ambao matokeo yake yalifutwa.

Viongozi hao, juzi walisalimiana na kupeana mikono wakiwa na bashasha katika dua maalum ya kuiombea nchi amani baada ya kumaliza uchaguzi mkuu na kuendelezwa kwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa (SUK). Sherehe hiyo iliandaliwa na Ofisi ya Mufti Zanzibar na kufanyika Msikiti wa Muwashawarra, Mwembe Shauri mjini Unguja.

Maalim Seif na Shein walikuwa hawapeani mikono baada ya kususia uchaguzi wa marudio wa mwaka 2016, kutokana na kufutwa kwa matokeo ya uchaguzi wa mwaka 2015.

Walipokutana katika msiba wa aliyekuwa Rais wa Zanzibar, Aboud Jumbe, Dk. Shein alimsalimia Maalim Seif kwa kumpa mkono, lakini alikataa na picha hiyo ilisambaa katika mitandao mbalimbali ya kijamii.

Akizungumza katika dua hiyo iliyohudhuriwa na viongozi mbalimbali, Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi, alisema viongozi wa kisiasa wana dhima kubwa mbele ya Mwenyezi Mungu na kusema maridhiano ya kisiasa yaliofanyika yameonyesha njia sahihi katika kudumisha umoja na mshikamano.

Alisema kuna umuhimu kwa wananchi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuwaongezea neema ya maridhiano yaliofanikisha uundaji wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa, baada ya uchaguzi mkuu kumalizika.

Dk. Mwinyi alisema viongozi wana dhima kubwa ya kuhakikisha wanadumisha amani na mshikamano, hivyo akatumia fursa hiyo kumpongeza Maalim Seif na chama chake cha ACT-Wazalendo kwa kukubali kushiriki katika SUK.

Alisema binafsi anaamini Wazanzibari wote ni kitu kimoja wakiwa na dhamira ya kuijenga Zanzibar, hivyo akawataka viongozi wa dini kuendelea kuwaombea dua viongozi ili waendelee kuiongoza nchi kwa ufanisi.

Dk. Mwinyi alisema wakati wa kampeni za uchaguzi mkuu uliopita, alitoa ahadi nyingi kwa wananchi ikiwamo ile ya kusisitiza kuendeleza amani na utulivu pamoja na kuwataka wananchi kuunga mkono juhudi za serikali katika kufanikisha azma hiyo.

Pia aliwataka Wazanzibari kufanya kazi kwa bidii kwa kila mmoja kutekeleza wajibu wake kikamilifu mahala alipo ili kuleta ustawi wa maisha ya wananchi.

Naye Katibu wa Mufti wa Zanzibar, Sheikh Khalid Mfaume, alisema dua hiyo inalenga kumshukuru Mwenyezi Mungu pamoja na kumwombea Rais Mwinyi na wasaidizi wake katika kutekeleza vyema majukumu yao ya kitaifa.

Viongozi waliohudhuria dua hiyo ni pamoja na Rais mstaafu Amani Abeid Karume, Balozi Seif Ali Idd, Mke wa Rais wa Zanzibar Mama Mariam Mwinyi, Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi Dk. Abdulhamid Yahya Mzee na Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar, Dk. Mwinyi Talib Haji.

# Mhadhiri ataka sheria moja kudhibiti vitendo vya ukatili

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MHADHIRI wa Sheria kutoka Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar, Sikujua Omar Hamdani, amesema wakati umefika kuwapo kwa sheria moja kwa ajili ya kupambana na udhalilishaji wa kijinsia.

Alisema hayo juzi katika maadhimisho ya Siku 16 za Kupinga Ukatili na Udhalilishaji ambayo yamewakutanisha wadau mbalimbali katika ukumbi wa watu wenye ulemavu Kikwajuni Mjini Unguja. Maadhimisho hayo yaliandaliwa na Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA) Ofisi ya Zanzibar. Sikujua alisema kuwapo kwa sheria ya pamoja ya kupambana na udhalilishaji wa kijinsia ni muhimu kwa kuwa itakusanya makosa yote yanayohusiana na vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia. Alisema sheria zilizopo sasa za makosa ya jinai zinakabiliwa na upungufu ambao kwa kiasi kikubwa hutoa mwanya kwa wahusika wa matukio hayo kuachiwa na kusababisha kuongezeka kwa wimbi la udhalilishaji wa kijinsia, ikiwamo ubakaji.

"Kuna mapungufu (upungufu) katika sheria zetu za kupambana na vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia. Tunahitaji kuwa na sheria moja ambayo itajikita moja kwa moja na matukio ya aina hiyo pamoja na adhabu zake," alisema. Sikujua alisema kuna umuhimu wa kuweka mkazo zaidi katika kufanya uchunguzi wa kesi za udhalilishaji wa kijinsia na ubakaji ikiwa pamoja na kuwekwa kwa muda maalumu ili kukamilisha uchunguzi na kesi kutajwa mbele ya vyombo vya sheria.

"Kesi za ubakaji zinachukua kuanzia mwaka mmoja hadi miwili kufanya uchunguzi kiasi cha wahusika kukata tamaa na kuona kwamba kesi yao tayari imetupwa," alisema. Baadhi ya washiriki wa mkutano huo, waliitaka jamii kubadilika na kuacha kufanya suluhu kesi za udhalilishaji wa kijinsia pamoja na kutoa ushahidi mbele ya vyombo vya sheria.

"Tunakabiliwa na tatizo moja kubwa la jamii wakati mwingine kufanya suluhu katika kesi za udhalilishaji wa kijinsia...wakati mwingine jamii haipo tayari kutoa ushahidi, hivyo kusababisha kesi kufutwa kwa sababu hakuna hatia bila ya ushahidi," alisema Khamis Mussa, Ofisa Upelelezi Makao Makuu ya Polisi Zanzibar. Naye Fatuma Juma kutoka Tume ya Kurekebisha Sheria, alisema wako katika mchakato wa kuhakikisha baadhi ya sheria zinapitiwa na kufanyiwa marekebisho baada ya kuonekana kutokidhi katika masuala ya kupambana na udhalilishaji wa kijinsia.

"Sitaki kusema sheria zipi zitafanyiwa marekebisho, lakini Tume ya Kurekebisha Sheria ipo katika mchakato wa kufanya mapitio ya sheria mbalimbali kwa lengo la kuona tunapambana na vitendo vya udhalilishaji," alisema.



**BELLE 9**

UKURASA 12

Nipashe
MWANGA WA JAMII

BT
BURUDANI TELE

JUMAMOSI DESEMBA 12, 2020



# 'SIJATUMIKA'

# Lucy aelezea siri ya urembo wake

MSANII wa filamu za tamthilia, Lucy Charles, ameamua kupasua ukweli kuwa yeye ni tofauti na waigizaji wengine, kwani mwili wake hautumiki ovyo na wanaume na ndiyo maana anakuwa mrembo muda wote.

Lucy ambaye alikuwa mshiriki wa Miss Tanzania 2010, akitokea Mwanza, amesema hawezi kuutoa mwili wake kama sadaka ili kupata madili ya fedha.

Amesema kuwa jamii inatakiwa kuelewa kutumika ovyo si chanzo cha kupata maisha mazuri, kwani mwanamke anaweza akatumika kwa wanaume na bado usifanikiwe kupata maendeleo yoyote.

"Mimi sijatumika, lakini siamini kama mtu anaweza akafanikiwa kwa sababu ya kutumika, pia unaweza ukatumika na usifanikiwe jamii inatakiwa ielewe kwani hiyo ni tabia ya mtu, sio lazima uwe staa unaweza ukatumika hata mtu wa kawaida na usipate maendeleo, naamini kwenye kufanya kazi na kutokata tama," ameeleza Miss Lucy Charles.

Ameongeza kwamba maisha yake yanakuwa halisi na kamwe hatoi nafasi kutafuta umaarufu kwa kutengeneza skendo kama wanavyofanya wengine.

Lucy amesema anapenda urembo wake na anaendelea kuthamini mwili wake kwa kuutunza vizuri kila wakati.

"Mfano katika kazi ya kupamba video kuna mambo mengi ya ajabu, lakini niliyakabili kutokana na mtu ukijua unataka nini na unataka kwenda wapi utafanikiwa kukabiliana na mazito," amesisitiza.

BASI SAWA

# Roma kweli unatuacha?

STAA wa muziki wa HipHop nchini, Roma Mkatoliki, ameachia ujumbe wenye utata kwenye mtandao wake wa Instagram na Twitter, ambao anasema wimbo atakaoutoa utakuwa wa mwisho kwake.

Roma ambaye kwa sasa anaishi nchini Marekani, kupitia ujumbe wake huo ameandika kuwa



"Wimbo wangu wa kwanza niliutoa mwaka 2007, wimbo wangu wa mwisho nitautoa muda wowote kuanzia sasa, na huu ndiyo utakuwa wimbo wangu wa mwisho, ahsanteni kwa kuni-support kwa kipindi chote cha miaka 13 nilichowahudumia kwenye sanaa hii ya muziki".

Kama atafanya hivyo, atakuwa msanii wa tatu kuamua kukaa mbali na muziki kwa mwaka huu, wengine ni Vanessa Mdee na Jolie.

# Smash sema ukweli kama unawachanganya

MTANGAZAJI wa East Africa Radio, King Smash amejikuta akitoa ufafanuzi kile kinachoendelea katika mitandao ya kijamii, akisema hafurahishwi kinachotokea.

Smash ameamua kutoa kauli hiyo baada ya kuwapo kwa uvumi kuwa anajihusisha kimapenzi na wanawake wawili tofauti ambao ni ripota wa shoo ya eNewz ya East Africa TV na Dolly Dolly mtangazaji wa The Base ya ITV.



"Sinamaoni yoyote kuhusiana na hilo, mimi huwa sizungumzii ujinga, pia siwezi kutolea ufafanuzi vitu vya kipuuzi na udaku, siwezi kukwazika wala kufurahi kwa kilichotokea kwani watu wanaingiza pesa kupitia mitandao ya kijamii wanatafuta 'content' kwa kuwazungumzia watu fulani ili wao wapate pesa hizo," amesema King Smash.



# Belle 9 amshukuru Ridhiwani kwa hili...

MWANAMUZIKI nyota wa RnB, Belle 9, ametaja siri ya mtoto wa Rais wa Awamu ya Nne, Dk. Jakaya Mrisho Kikwete, kumpatia nyumba kwa ajili ya uzinduzi wa wimbo wake mpya.

Amesema, Ridhiwani Kikwete, ambaye ni Mbunge wa Chalinze alimpatia mjengo huo uliopo eneo la fukwe ya Mikocheni, ili kufanyia sherehe ya uzinduzi wa video ya wimbo wake wa 'give it to me' bila malipo.

"Namshukuru sana Mh Ridhiwani Kikwete kwa sababu sijawahi kupata sapoti yoyote kutoka kwa mwanasiasa wa chama chochote kunifanyia kitu kikubwa kama kile, kiukweli Mungu ambariki sana, aliweza kunipa 'beach house' yake ya Mikocheni kufanya uzinduzi wa video yangu, ilikuwa kama zawadi na kitu kikubwa kwangu sitaweza kusahau." ameeleza Belle 9.

# Mrembo Kipofu: Mwisho wa Ubaya Aibu

**Na Adam Fungamwango**

UNAWEZA ukazitaja methali kibao za kiswahili kama vile 'malipo hapa hapa duniani', 'ubaya hauna cheo', na vyovyote vile, lakini lengo ni moja tu kufikisha ujumbe kuwa mtu yoyote anayefanya ubaya, haujawahi kumuacha salama hapa hapa ulimwenguni.

Kuna watu duniani huwafanyia ubaya wenzao ili wanufaike, au kuona wenzao wakiadhirika, au kwa sababu ya ubinafsi tu ya kile kitu cha mwenzake kukitaka yeye, hata kama si halali kwake.

Ukiitazama filamu ya 'Kipofu Mrembo' utajifunza vitu vingine vinavyohusiana na hulka ya baadhi ya binadamu kuwafanyia wenzao ubaya bila ya hofu ya Mungu.

Ni filamu yenye kusikitisha, majonzi, lakini ina mafunzo kwenye jamii yetu hii ambayo watu wema wamekuwa wakipungua duniani kadri muda unavyozidi kusonga mbele.

Imechezwa Pemba, Zanzibar, pamoja na Dar es Salaam, ikiwashirikisha baadhi ya nyota kadhaa nchini kama Haji Adam, Riyana Ally na Fadhili Msisiri.

Mzee Msisiri ana binti yake mrembo aitwaye Rau. Ni binti mwenye sifa zote za mwanamke mrembo. Lakini ni kipofu. Ulemavu huu unafanya wanaume wengi waogope kumuoa kutokana na kuogopa changamoto watakazozipata.

Salim, mtoto wa mzee Mwinyi, anamweleza waziwazi baba yake kuwa hataki kumuona binti huyo, baada ya mzee wake rafiki wa Msisiri kukubaliana waozeshane.

Kijana mmoja kutoka mjini anarudi kijijini kwao Pemba akiwa anaendesha gari na




kutaka kumgonga binti mmoja njiani. Anagundua kuwa ni kipofu. Anampa lifti na kumrudisha kwao. Lakini anatokea kumpenda. Anamuoa na kwenda naye kuishi mjini. Katika kumsimulia jinsi alivyopata upofu kuwa haukuwa wa kuzaliwa, Athumani anaamua kumpeleka hospitali na madaktari wanamhakikishia kuwa akienda kwenye hospitali kubwa za Dar es Salaam atapona.

Wanafika Dar na kweli mrembo huyo anapona. Lakini badala ya kuwa furaha, ingawa kama majonzi.

Kuna watu sasa wakawa wanamtaka mrembo huyo. Kwa kuwa sasa ana macho. Licha ya gharama alizoingia Athumani ikawa bure. Jamaa mmoja anaitwa Ebby alimtaka sana Rau, lakini demu alikuwa hataki. Alichofanya ni kumfanyia fitina Athumani afukuzwe kazi, lakini akaenda kwa mganga ili mwanamke amkubali. Athumani anafukuzwa kazi na ghafla Rau anaomba talaka kwa mumewe na kutimkia kwa Ebby.

Dawa ya moto ni moto, mzee Msisiri anaamua naye kwenda kwa mganga ili binti yake amtoroke Ebby na kumrudia mumewe wa zamani ambaye alimfanya kuona. Dawa kwa Ebby zinakufa nguvu. Rau anamkimbia Ebby na kumrudia mumewe Athumani.





# Duuh! Hata Beka uliulizwa swali hili?

MJADALA unaondelea kuhusu kwa nini idadi kubwa ya wanawake wanaamini mwanaume anakuwa wa kwanza kufariki, unazidi kushika kasi na sasa watu maarufu wamejikuta wakitoa maoni yao.

Kupitia kipindi cha PlanetBongo kinachorushwa na East Africa Radio, ilimnukuu mke wa msanii Beka Flavour, Happiee Reuter, akikiri hata yeye aliwahi kumuuliza mumewe endapo akitangulia ataiachaje familia yake.

"Wanawake tunapenda kuuliza hilo swali kwamba mume akifariki itakuaje kwa sababu tunapenda kufikiria future zaidi, wao wanafikiria leo tu kwa hiyo lazima ujiongeze, niliwahi kumuuliza mara moja nikaona majibu yake siyaelewi," amesema.

# NGOMA 5 ZA NZAYADIO ZILIZOWACHENGUA WABONGO

**Na Adam Fungamwango**

SI Wakongomani tu waliosikitishwa na kifo cha mkongwe wa muziki wa dansi, Nzaya Nzayadio aliyefariki nchini Uingereza, bali hata Wabongo.

Kwenye baadhi ya vyombo vya habari na mitandao ya kijamii kulizuka maneno ya huzuni na masikitiko baada ya kutangazwa kifo chake.

Mwanamuziki huyo alifariki Dssemba 7 kwenye Hospitali ya Hull Royal Infirmary mjini Hull City nchini Uingereza, alipokuwa amelazwa kiasi cha wiki mbili akiugua ugongwa na COVID-19, unaosababishwa na virusi vya corona.

Ana historia kubwa kwenye ulimwengu wa muziki, lakini umaarufu wake ulianza mwaka 1973 alipojiunga na Orchestra Lipua Lipua kwenda kuziba sauti ya Pepe Kalle aliyekuwa amejiengua na bendi hiyo kwenda kuunda bendi yake ya Empire Bakuba.

Hadi anafariki mwanamuziki huyo alikuwa akiishi nchini Uingereza, akiendelea na mambo ya muziki, lakini alikuja nchini Tanzania miaka michache tu iliyopita akiwa mwenyeji wa mwamuziki mwenzake Tshimanga Kalala Assosa ambaye walikuwa wote kwenye bendi ya Lipua Lipua, kabla ya kina Assosa kwenda kuunda Les Kamale.

Ni mwimbaji mwenye sauti nzito, ambayo ukiisikiliza inashabihiana na ya Pepe Kalle au Madilu. Nchini Tanzania mashabiki wa muziki wameonekana kusikitishwa na kifo hicho kutokana na kuzipenda sana nyimbo za Lipua Lipua hasa kuanzia miaka ya 1973 hadi katikati ya miaka ya 1980.

Hizi ni nyimbo ambazo ziliimbwa na mwanamuziki huyo na kupendwa mno na mashabiki wa muziki wa cavasha nchini Tanzania na ndizo zilizowaliza wengi waliposikia kifo cha Mkongomani huyo mwenye sautio ya kushiba.

**Sekizengi**

Hizi ndizo nyimbo za mwanzo kabisa za Nzaya Nzayadio kutunga na kuimba kwenye bendi hiyo na kuwasahauliza mashabiki kuondoka kwa Pepe Kalle ndani ya bendi hiyo.

Ukiusikiliza wimbo huo, kwenye tambulisho wake, kabla hata hajaanza kuimba yeye na wenzake, anaanza kusema maneno yafuatayo 'Nzaya Nzayadio na Sekizengi'. Ni mmoja wa wimbo maarufu sana nchini na ulipendwa na mashabiki wengi.

**Kendeke Malembe**

Huu nao ni mmoja kati ya nyimbo zilizompatia sifa sana mwanamuziki huyo aliyefariki nchini Uingereza aliyefariki akiwa na miaka 65.

'Kendeke Malembe' ni kati ya nyimbo bora kabisa za Lipua Lipua ambazo mwanamuziki huyo aliziimba kwa ufundi wa hali ya juu.

Anaimba sauti ya tatu kwa sauti nzito akimbeba mwimbaji wa sauti kali ya kwanza, Kilola Tokodiangani ambaye bado yupo hai.

**Mfueni**

Ukitaka kusikiliza kazi halisi ya marehemu Nzaya, msikilize kwenye wimbo na 'Mfueni' ni wimbo ambao umepigwa kwenye hali ya masikitiko na huzuni. Waimbaji na vyombo vyote vimepigwa katika hali ya masikitiko. Nzaya anaghani kwenye ufundi wa hali ya juu, kiasi kwamba yoyote aliyeguswa na msiba huu, atamfikiria marehemu pamoja na wimbo huu jinsi alivyoimba.

**Matoba**

Ni wimbo ambao haya yeye mwenyewe aliupenda sana. Hata alivyokuwa Uingereza, alijaribu kuuingiza kwenye teknolijia ya kisasa kwa kurekodi video yake na kuitoa upya, kiasi cha hata vijana wa kisasa nao kutazama ufundi wake.

'Matoba' ni moja kati ya nyimbo kali ambazo marehemu aliziimba kwa hisia kali pia.

**Nouvelle Generation**

Sidhani kama kuna aliyekuwa kijana au mtoto miaka ya 1970 ambaye haufahamu wimbo huu. Ndiyo mmoja wa nyimbo maarufu zaidi si za bendi ya Lipua Lipua tu, bali zote za mtindo wa Cavasha kutoka nchini Zaire wakati huo na sasa Congo.

Hata wachambuzi wa muziki walipokuwa wakitoa habari ya msiba wa mwanamuziki huyo, wimbo huu ndiyo ulitumika.





# Duncan wenzio wanafanyaga siri

STAA wa muziki kutoka Nigeria, Duncan Mighty, amemshutumu mke wake, Vivien kwa kutokuwa mwaminifu katika ndoa baada ya uchunguzi wa vinasaba kubaini binti yao, Mitchell sio wake.

Katika ujumbe wake mrefu aliouweka katika ukurasa wake wa chapisho lingine refu lililoshirikiwa kupitia ukurasa wake wa Instagram, mwanamuziki huyo alimtaja Frank, kuwa ndiye baba wa Mitchell.

" FRANK ni rafiki mzuri sana na ni baba wa Mitchell kwani DNA imenithibitisha, mke wangu amekosa uaminifu na kusababisha majuto katika moyo wangu," amesema.



## Ubi mbona unajishtukia?

Mwanamuziki Ubi Franklin, amesema kupata watoto wanne kwa mama tofauti si dhambi na kwamba hataonekana mtu mbaya katika jamii.

Katika ujumbe wake wa Twitter, msanii huyo ambaye ni mjasiriamali, amesema suala hilo pia halimfanyi kuwa na uhusiano mbaya na wazazi wenzake.

"Nimefikisha miaka 34, huwezi kunihumu na kuniita majina mabaya kwa sababu tu nina watoto wa nje kutoka kwa wanawake wazuri. Kutofunga ndoa huwezi kuonekana mtu mbaya katika jamii," amesema.

## Kilio cha Davido, machozi ya wote

MSANII mkali wa muziki nchini Nigeria. David Adeleke, maarufu kama Davido, ameandika ujumbe wa majonzi baada ya mlinzi wake wa kibinafsi, Ogbeide Tijani Olamilekan, kufariki dunia.

Katika ukurasa wake wa Instagram, Davido, aliweka ujumbe huo ambao ulimmwagia msifa mlinzi wake huyo aliyefahamika kama TeeJay.

"Tafadhali niambie naota ... Tj wangu ameenda? Je, mimi nitafanya nini bila wewe mjomba Tj ehn? Miaka 11 ulinifanyia yote, uliniweka mbele yako kila wakati," ulisema sehemu ya ujumbe huo.





## Tacha unachosema kina maana

ALIYEKUWA mshiriki wa Big Brother Naija, Natacha Akide, maarufu kama Tacha, amewashauri watu kuacha kuwaona wanawake kama wahitaji wakubwa wa ndoa zaidi ya wanaume.

Akitumia ukurasa wake wa Instagram, Tacha amesema jambo hilo halikubaliki kwani wote wanahitaji suala hilo kwa usawa.

"Acha kushinikiza kwamba wanawake wanahitaji jambo hili la ndoa kuliko wanaume. Sio jambo kubwa kwetu kama mnavyoamini," ameandika.

## Aniola unajichuria ujue

STAA wa filamu kutoka Nollywood, Eniola Badmus, amewashauri watu kuacha kuuchukia mwili wake ili wasimsababishie kifo cha mapema.

Mwigizaji huyo aliandika ujumbe kupitia ukurasa wake wa Instagram, kuwa tabia za watu kuanza kumsema vibaya mwili wake ni sawa na kumtakia kifo kutokana na kuwa na mawazo mengi.

"Mwili ni ule ule ninao ambao mnaouchukia, ni mwili ule unaoweka chakula mezani kwangu na unaoleta furaha kwako unapoiangalia runinga, acheni kunisema ili msiniue mapema," ameandika.



HABARI MAKALA

# Tuzo za wanamabadiliko zitaleta ukombozi




Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Zainab Telack (kushoto), ambaye ni miongoni mwa machampioni 16 waliopewa tuzo hizo, akiwa kwenye picha ya pamoja na machampioni wengine waliopewa tuzo hiyo na Shirika la Wanawake katika Sheria na Maendeleo Afrika (WiLDAF) kwa kushirikiana na Shirika la Kimataifa la Mpango wa Chakula Duniani (UNFPA). **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

**Na Joseph Mwendapole**

SIKU 16 za Kupinga Ukatili wa Kijinsia zimekuwa zikitumiwa na wanamabadiiko kuelezea umuhimu wa kuchochea harakati za kupinga ukatili wa kijinsia ambao unaelezwa kuongezeka hapa nchini.

Asasi mbalimbali zimekuwa zikiadhimisha siku hizo 16 nchini kote kwa kufanya matukio mbalimbali kama kutoa msaada wa sheria kwa watu wasio na uwezo na kutoa elimu ya ukatili wa kijinsia.

Shirika la Wanawake katika Sheria na Maendeleo Afrika (WiLDAF) kwa kushirikiana na Shirika la Kimataifa la Mpango wa Chakula (UNFPA) walikwenda mbali zaidi kwa kuamua kuanzisha tuzo zinazoitwa za machampioni wa mabadiliko.

Watu 16 waliofanya mambo makubwa walitunukiwa tuzo hiyo ambayo imetolewa mwaka huu kwa mara ya kwanza na ambazo zitakuwa zikitolewa kila mwaka kama sehemu ya kuongeza chachu ya mapambano dhidi ya uovu wanaofanyiwa wanawake na watoto wa kike.

Miongoni mwa waliotunukiwa tuzo hiyo ni Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Zainab Telack, ambaye anaelezwa kuwa mstari wa mbele kupambana na ukatili dhidi ya wanawake hasa vikongwe.

Alipopewa nafasi ya kuzungumza alitoa siri ya aliyofanya hadi kuonekana anafaa kupewa tuzo kwamba ni kupambana na wanaoua vikongwe wenye macho mekundu kwa imani za kishirikina.

Anasimulia kuwa alipoteuliwa tu mwaka 2016 kuwa Mkuu wa Mkoa huo, alianza kupambana na vitendo vya mauaji ya wanawake wazee walioonekana kuwa na macho mekundu na alifanikiwa kwa kiasi kikubwa.

"Nilipoteuliwa tu nilisema sitalala mpaka nitokomeze mauaji haya ya vikongwe na kwa kweli tulijipanga mimi na Mkuu wa Jeshi la Polisi Mkoa tumefanikiwa hivi sasa Shinyanga ni salama kwa uwekezaji makazi na huwezi kusikia tena mauaji ya wanawake wazee," alisema.

Kuhusu mimba za wanafunzi RC anasimulia kuwa walifanya kampeni kubwa kuwakamata wote waliokuwa wakioa au kuozesha wanafunzi na hivi sasa idadi kubwa ya wanafunzi wa kike mkoani humo wanahitimu masomo yao bila kupata ujauzito.

Anasema yeye na timu yake walifanya kampeni ya kuchunguza kila harusi inayofanyika mkoani humo na wanapokuta anayeoa au kuolewa ni mwanafunzi waliwachukua wote waliokuwa wanahusika kwenye sherehe hizo na kuwafikisha kwenye vyombo husika kwa hatua zaidi.

"Tulikuwa tunapita shuleni kuangalia mahudhurio ya nani hayupo, yuko wapi na anafanya nini, tuliwafuatilia wote tukahakikisha walioacha shule wanarudi na wale waliopanga kuolewa tulivuruga mipango yao na sasa wengi wako shuleni wanaendelea na masomo," anasema.

Mkuu huyo wa Mkoa anasisitiza kuwa wazazi lazima wahakikishe wanawalea watoto wao kwenye maadili mema kwa kufuatilia mienendo yao badala ya kuwaacha wakizunguka zunguka bila mpango.

Anasema baadhi ya wazazi wamewaacha watoto wao walelewe na jamii kwani hawana muda wa kufuatilia mwenendo wa mtoto wake siku nzima.

Mkurugenzi wa WiLDAF, Anna Kulaya, anasema tuzo hizo ambazo zimezinduliwa mwaka huu zitakuwa zikifanyika kila mwaka kwa ajili ya kuwatambua watu waliofanya vizuri zaidi kwenye mapambano dhidi ya vitendo vya ukatili wa kijinsia.

Anasema kuna ukatili mwingi unaotokea kwa wanawake ukiwamo ubakaji kwa wanawake na wasichana ndiyo maana mwaka huu WiLDAF imeamua kuangalia pia jitihada zinazofanywa na watu wa kawaida kabisa kupambana na ukatili wa kijinsia na kupata mafanikio.

"Getrude Mongela ametuzindulia hizi tuzo na ametoa mapendekezo kwa Rais wetu kwamba kama ana uwezo wa kutoa elimu bure na kujenga miradi mikubwa yenye manufaa kwa nchi basi anaweza pia kusema basi kwa unyanyasaji wa wanawake na tunahamu kumsikia rais wetu akikemea kwa sauti kubwa ukatili wa wanawake," alisema.

Anasema ingawa ukatili wa kijinsia bado uko nchini, lakini kuna umuhimu wa kujenga utamaduni wa kuwatambua watu waliofanya vizuri zaidi kwenye mapambano ya kuwalinda wanawake na wasichana.

Anasema hatua hiyo itasaidia sana kutoa changamoto kwa watu na makundi mengine kuona umuhimu wa kuchukua hatua kupambana na vitendo vya ukatili wa kijinsi maeneo yote nchini.

"Hawa waliopata tuzo hizi si kwamba walipatikana kirahisi tu hapana, walipitia mchujo mkali sana kwa sababu walikuwa maelfu kwa maelfu hivyo kupatikana kwao kumekuja baada ya hawa kuonekana kwamba walikuwa vinara zaidi," anasema.

Anasema baadhi ya watu waliopata tuzo wanatoka kwenye maeneo ambayo yana mfumo dume uliokita mizizi, lakini wamefanikiwa kubadili mitazamo ya watu kuhusu mwanamke.

"Hawa watu ni alama kwetu kwamba inawezekana kabisa kwa jamii kubadilika na kubadili mitazamo hasi ndani ya jamii inayosababisha kuendelea kwa vitendo vya ukatili dhidi ya wanawake na kutozingatiwa kwa usawa wa kijinsia," anasema.

Balozi Getrude Mongela ambaye alikuwa mgeni rasmi kwenye uzinduzi na ugawaji wa tuzo hizo alisema wanawake wanapaswa kusimama na kuendeleza mapambano badala ya kulialia.

Aliwashangaa wanaume ambao bado wanaendeleza vitendo vya ukatili wa kijinsia akiwataka kuachana na tabia hiyo iliyopitwa na wakati na kuwaacha wanawake waishi maisha ya staha.

## MIAKA 58 YA UHURU

# Mjue 'rafiki ndugu' wa Nyerere kupika, kupakua utoto hadi kifo

## ●Shamba pamoja, wapinzani wa bao...

**Na Peter Orwa**

UNAPOKAA chini kumtafakari Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere na nyendo zake ana mengi. Mfumo wa maisha yake aligawanya katika mipaka miwili mikuu, binafsi na saa za kazi na daima hazikufanana.

Nipashe wiki hii katika safu yake ya toleo la kilele cha Siku ya Uhuru wa nchi, ilidokeza namna walivyokuwa pacha wa kazini na Mzee Rashid Kawawa, pia nyumbani nako si haba, hawakuwa mbali kabla na baada uhuru, hadi kustaafu.

Panapo kujua maisha yake binafsi nyumbani, mbali na ya kazini, yuko wa karibu yake anayeweza kubeba sifa nyingi anayetambulishwa kuwa mdogo wake, binamu au rafiki, ndio utambulisho unaoonekana kumkaa zaidi.

Huyo ni Mzee Nyang'ombe Warioba, aliyedumu kuwa mbia wake mkuu kila walipokuwa nje ya ofisi, akimjua kwa kina Mwalimu Nyerere, tabia, historia yote na hata kumuiga sauti yake kwa ufasaha.

Ni mwanahabari na aliyekuwa mkuu wa wilaya, marehemu Muhingo Rweyemamu, aliniuzia wazo kwa kunidokeza pindi nitakapohabatika kufika Butiama, kuna mwenye mengi ya kupendeza na yaliyojificha, yanayomhusu Mwalimu Nyerere katika zama hizo akiwa hai, wastani wa miaka 22 sasa.

Ulitimu wakati nikiwa kijijini Butiama kumtembelea Mama Maria Nyerere kwa ziara ya kikazi, katika orodha ya azma yangu ilikuwamo kumpata Mzee Nyang'ombe Warioba.

Siku iliyofuata baada ya kukutana na mama huyo, nilianza safari ya kutumia baiskeli umbali wa kilomita saba Kaskazini Mashariki kutoka kijijini Butiama, kwenda kijijini Muryaza.

Ni katika makazi njia kuu iendayo katika tawi dogo la Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), Buhemba nikiwa na mwenyeji wangu tuliwasili kwa Nyang'ombe, ambaye hakuwa na kikwazo cha mazungumzo hayo.

UPENZI WA BAO

Mzee Nyang'ombe ambaye anajitambulisha kuwa karibu na Mwalimu Nyerere maisha yote, tangu utotoni pasipo kuachana hadi umauti. Alisema alikuwa na umri chini ya binamu yake huyo kwa tofauti ya miaka saba, lakini 'waliiva' katika sura ya marafiki.

Anasema, moja ya kilichowaunganisha tangu zama hizo ututoni ni ushindani wao katika mchezo wa bao na hili liliendelea hata Nyerere alipoenda mbali masomoni, kila alipofika kijijini ushindani wao ulikuwa katika bao.

Huku akitambulisha mchezo huo kupendwa kupita kiasi na Mwalimu Nyerere, Nyang'ombe alisimulia mkuu huyo wa nchi alipoingia madarakani, alijenga utaratibu wa kumualika jijini Dar es Salaam.

Alisema, pindi alipokuwa jijini Dar es Salaam, Mwalimu Nyerere aliishi Msasani na Nyang'ombe mjini na pindi Rais alipofika tu nyumbani kutoka kazini, aliagiza usafiri wa kumpeleka Nyang'ombe haraka.

Mzee huyo kutoka kijijini Muryaza alisimulia kila walipokutana walijumuika kwa 'michapo' hawakuacha kushindana katika mchezo bao, anaokiri walikuwa na ushindani mkali.



Mzee Nyang'ombe Warioba (kushoto), akiwa na msomi mtafiti kutoka Chuo Kikuu cha Edinburg, cha Uingereza, Dk. Thomas Molony (katikati), aliyefika kijijini Muryaza, kupata habari za kina za Mwalimu Nyerere, aliyesoma masomo ya uzamili katika chuo hicho. Ilikuwa mwaka 2010. Kulia ni mtoto wa Nyang'ombe.

Alimweleza Nyerere kwamba alikuwa 'mbishi' katika ushindani na hasa kila alipofungwa alitaka bao kuendelea akisaka ushindi kuna wakati walifika hata saa sita usiku.

Nyang'ombe aliendeleza simulizi kwamba ilifika hatua kwamba, hata wasaidizi wake waliingilia kati kumnong'oneza Nyang'ombe pindi Mwalimu alitoka kidogo, wakimtaka akubali kufungwa, ili mkuu wa nchi aridhie kwenda kulala.

"Aliporudi, nilimwambia 'eti hawa (wasaidizi) wananiambia kubali kufungwa ili ukapumzike, lakini alikataa na akawaambia 'nendeni mkalale, sisi tupo...'' alisimulia.

Ni tabia aliyoieleza, kudumu hata baada ya kustaafu na kuweka makazi kijijini Butiama, Mwalimu Nyerere alibobea zaidi katika bao, kwani wakati huo alikuwa na muda wa ziada na ushindani wao mkuu.

Akiwa Butiama, alisema Nyerere alikuwa na mbwembwe zaida, kwani walikuwa na mazoea ya kucheza jioni wakati walikuwa na ushindani mkali, basi Mwalimu Nyerere alikuwa na mbwembwe ya kuwanunulia soda mashabiki wote waliowazunguka kuona mchuano kijijini.

Kipindi hicho pia, Mwalimu Nyerere, alikuwamo katika kamati mbalimbali za siasa za kimataifa na ilipotokea amesafiri na siku ya mwisho alifungwa katika mchuano wa bao aliondoka na 'usongo.'

Nyang'ombe alisema, alionyesha alikuwa amepania kulipiza kisasi cha kufunga, kwani aliporejea tu, aliagiza gari hadi kijijini Muryaza kumfuata Nyang'ombe, wakachuane Butiama na alihamia huko hadi Nyerere aliopopata safari nyingine.

"Utamsikia, nimetoka Sweden! Wewe unakujua? Njoo hapa nikufunge," anasimulia alivyokumbuka majigambo yake, akiendelea kwamba:

"Sikuwa na tabu ya kujua kama amerudi. Nikiona gari hilo linakuja, najua amerudi na hata kijijini (Murayaza) wenzangu walipoona gari, walinitania, rafiki yako (Nyerere) ameshakuja,"

Kwa mujibu wa Nyang'ombe, kila Mwalimu Nyerere aliporejea Butiama, yeye alihamia huko kwa muda wote na walidumu pamoja, ikiwamo mashamba yao walilima kwa kushirikina kwa kutumia jembe la mkono, wakianza na shamba la mmoja na kisha wanahamia la mwingine.

Nyang'ombe, anamtaja kijana msaidizi wa nyumbani Butiama naye alikuwa rafiki kipenzi mwingine, waliochangia maisha ya mazungumzo na masihara.

Mwandishi alimdadisi, je, ni kila kitu Nyerere 'alimkubali'? Nyang'ombe, alijibu 'hapana.' Alitoa mfano pindi aligundua ametumia pombe na ina namna ya kumwelemea, alimwambia kwa ukali wa kaka, akimkariri kwa ufasaha sauti aliyotamka: "Wewe naona leo hauko vizuri, kalale tutaonana kesho!"

Nyang'ombe anasema, kutokana na msimamo huo wa kaka yake, naye alijenga tabia ya kumkwepa asimkere pindi anapokuwa katumia kinywaji, ili asimkere.

Ndugu huyo anaeleza Nyerere, maishani alikuwa na upekee wa kutokunywa maji sana, alitumia kidogo na hata kuna wakati walitoka shambani, yeye alikunywa maji mengi, lakini Mwalimu Nyerere alitumia kiasi kidogo sana na kuridhika.

Ni katika maisha yote aliyomfahamu Mwalimu Nyerere, Nyang'ombe alimweleza alikuwa hakuwa na hulka ya kulipiza kisasi na marafiki zake walikuwa watu wa chini.

Hata aliporejea kumbukumbu wakati alipokuwa katika harakati za kusaka uhuru, Nyerere alikuwa kila anapotokea kurejea nyumbani, hakuwapa maelezo mengi ya wanayoyafanya huko, baada yake alijikuta na urafiki wa likizo.

"Tulimuuliza vipi huko, mtafanikiwa? Alitujibu acheni, mnajua nyinyi?" Alisimulia Nyang'ombe, ambaye wakati anaongea na mwandishi akiwa na masikitiko yake ambayo yalimwacha katika kitendawili.

Nyang'ombe alisema, muda mwingi walikuwa na mdogo wake marehemu Kiboko Nyerere, ambao mara kadhaa walienda Arusha na kisha walirejea Butiama.

Alisema, wakati Mwalimu Nyerere anaondoka kwenda Uingereza kutibiwa, alimuita na kumnong'oneza kwa kauli "nikirudi kuna jambo nataka kuongea nawe" safari ambayo hakurudi hai, mwaka 1999.

Kwa taarifa ambayo Nipashe iliambiwa karibuni kutoka katika familia, ni kwamba Nyang'ombe naye ni marehemu sasa, kama walivyo Kiboko na baadhi ya ndugu wa umri wake, ambao wana utajiri wa simulizi za Mwalimu Nyerere ambazo mwandishi alifaidika nazo.

● **Ni faragha ya mazungumzo ambayo mwandishi alipata miaka 18 iliyopita, vijijini Butiama na Muryaza, Mara. Mungu azilaze roho zao mahali pema. Amina.**



Mwalimu Julius Nyerere, akishiriki mchezo alioupenda zaidi. **PICHA ZOTE: MTANDAO**



Aliyekuwa Spika wa Bunge la DRC, Jeanine Mabunda, akizungumza baada ya kupigiwa kura ya kuvuliwa nafasi hiyo juzi. **(PICHA: AFP)**

# Trump ajiandaa kuondoka Ikulu, aidhinisha mtu mweusi kunyongwa

**WASHINGTON, Marekani**

KUTEKELEZWA kwa hukumu ya kifo kwa Brandon Bernard, itakuwa taswira mbaya kwa Rais wa Marekani, Donald Trump, ambaye ana siku chache kabla ya kuondoka Ikulu ya nchi hiyo.

Hukumu hiyo ilitekelezwa katika Jimbo la Indiana, baada ya ombi la dakika za mwisho la kukata rufani kukataliwa na Mahakama Kuu ya Marekani

Bernard (40), alihukumiwa kwa makosa ya mauaji mwaka 1999 wakati akiwa kijana mdogo, na amevunja rekodi kuwa mhalifu mdogo kuhukumiwa kifo kwa zaidi ya miaka 70.

Kabla ya kuchomwa sindano ya sumu, Bernard aliomba msamaha kwa familia ya watu aliowaua.

Hata hivyo, hukumu nyingine nne za vifo zimepangwa kutekelezwa kabla Rais Trump hajaondoka madarakani.

Ikiwa watu wote watano watanyongwa, basi utawala wa Trump utakuwa umeidhinisha vifo katika kipindi cha zaidi ya karne moja. Tangu mwezi wa Julai watu 13 wamenyongwa.

Bernard alitangazwa kuwa amekufa saa 3:27 usiku za Marekani, sawa na siku ya Alhamisi, saa 5 asubuhi katika Gereza la Terre Haute.

"Ninaomba radhi. Haya ni maneno pekee ninayoweza kusema kuelezea namna ninavyojisikia sasa na namna nilivyojisikia siku hiyo," alisema, kwa mujibu wa shirika la habari la Associated Press.

Utekelezaji wa hukumu ya kifo ilicheleweshwa kwa zaidi ya saa mbili, baada ya mawakili wa Bernard kuitaka Mahakama Kuu kusitisha, lakini ombi hilo lilikataliwa.

Bernard alipewa adhabu ya kifo kwa kuhusika kwake na mauaji ya watu wawili, Todd na Stacie Bagley mnamo Juni mwaka 1999.

Kabla ya mauaji hayo, yeye na wenzake wanne wanaotuhumiwa kuwaibia marehemu hao na kuwalazimisha kukaa nyuma ya gari lao.

Kisha walipigwa risasi kwenye gari na mwenzao Christopher Vialva (19) kipindi hicho, kabla ya Bernard kulichoma moto gari.

Mawakili wa utetezi wanasema wote wawili walifariki kabla ya gari kuchomwa moto.

**BBC**

# Morocco kurejesha uhusiano na Israel

**RABAT, Morocco**

KUMEKUWAPO na maoni mchanganyiko tangu Morocco na Israel kutangaza makubaliano ya kurejesha mahusiano ya kidiplomasia.

Hatua hiyo imekuja baada ya juzi Marekani kutangaza kuitambua Sahara Magharibi kuwa ni sehemu ya Morocco.

Rais wa Misri, Abdul Fattah al Sisi, aliipongeza hatua hiyo, huku Chama cha Hamas kinachoongoza Ukingo wa Gaza, kuuita ni usaliti kwa dhamira ya Wapalestina.

Chama cha Polisario kinachopigania uhuru wa Sahara Magharibi, kimelaani vikali hatua hiyo ya Marekani kwa kuizawadia ardhi yao kwa Morocco, na kuiita kuwa haki isiyokuwa yake.

Morocco linakuwa taifa la nne la Kiarabu kuwa na uhusiano wa Kidiplomasia na Israel, ndani ya kipindi cha miezi minne, na kuachana na msimamo mkali wa miongo kadhaa wa kuitenga.

Kampeni ya kuyashawishi mataifa ya Kiarabu kukubaliana na Israel inaongozwa na Marekani, ikiwa kama njia ya kuunda muungano wa kukabiliana na hasimu wao mkubwa Iran.

**DW**

# Spika wa Bunge DRC aondolewa madarakani

**KINSHASA, DRC-Congo**

WABUNGE 281 wa Bunge la nchi ya Jamhuri ya Demokrasia ya Congo, wamepiga kura ya kumwondoa madarakani Spika Jeanine Mabunda, katika mgogoro wa kuwania madaraka unaoendelea nchini humo.

Jumla ya wabunge 484 walihudhuria kikao kilichoketi juzi, ambacho kilikuwa maalumu kumwondoa Spika ambaye ni mfuasi wa aliyekuwa Rais wa nchi hiyo, Joseph Kabila. Wabunge wengine 200 walipinga uamuzi huo.

Hatua ya kuondolewa madarakani spika huyo, inampa nguvu Rais Felix Tshisekedi, kuwa na sauti katika kuongoza serikali baada ya mtafaruku unaondelea kuwania madaraka kati yake na wafuasi wa Kabila. Wabunge wa Kongo wamechukua uamuzi huo baada ya kumshutumu Spika, Mabunda kwa kuegemea zaidi itikadi za kiasiasa katika uongozi wake na kutokuwa muwazi katika usimamizi wa fedha za chombo hicho.

Hata hivyo, spika huyo alikana shutuma zilizotolewa dhidi yake na aliomba radhi kutokana na hali ya kutoelewana iliyojitokeza. Awali, aliwasihi wabunge kulikataa pendekezo lililowekwa dhidi yake na wafuasi wa Tshisekedi kwa sababu za kisiasa.

Ushindi huu wa wapinzani wa Kabila, ni ishara ya kuimarika nguvu kwa washirika wa Rais Tshisekedi, ambao kwa sasa wanaweza kuwa na wingi wa kutosha ikilinganishwa na Baraza la Mawaziri ambalo wengi wanatoka upande wa Kabila.

Kura hiyo imepigwa baada ya siku kadhaa za ghasia ndani ya bunge hilo, hatua iliyosababisha polisi kuingilia kati ili kuituliza hali ya mambo.

Wafuasi wa Kabila wa muungano wa kisiasa wa FCC walimshukutu Tshisekedi kwa kukiuka katiba.

Chama hicho kilisema Tshisekedi anapanga njama za kuanzisha utawala wa kidikteta.

"Kila kitu ambacho tumefanya hapa kimekuwa na msingi wa kitapeli. Kwa kweli tulilazimika kulikataa hili na hatukupaswa hata kupiga kura," alisema Paulin Kashomba ambaye ni mfuasi wa Kabila.

Mfuasi wa Rais Tshisekedi, Jose Ngulamulumbe, alisema sasa wanafuraha kwa sababu Mabunda ameondolewa kuongoza bunge na kwamba siasa za Kabila sasa hatimaye zinaondoka.

**DW**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## VIWANJA/MASHAMBA

**PATA MKOPO WA HARAKA KWA MASHARTI NAFUU KUTOKA EFL**
Mkopo umelenga dharura na mahitaji mengine kama vile:
- **Kuboresha biashara**
- **Kulipa kodi ya nyumba**
- **Kumalizia tenda**
- **Kulipa matibabu n.k.**

Mawasiliano yetu:
**Dar es salaam – 0768 928 516.**
**Arusha – 0677 226 960.**

## NAFASI ZA KAZI

**Nafasi za kazi ya ualimu Diploma**
**- Kiswahili**
**-Science SST**
**- Kiingereza**
**Mawasiliano:**
**0783 334653**

## NAFASI ZA SHULE

**Keland Nursery and Primary School iliyopo Salasala Rtd inatangaza Nafasi Za Awali Na Msingi. Mawasiliano : 0713327613.**

NIPASHE NI JIBU LAKO
NJOO UTANGAZE NASI
KWA BEI NAFUU SANA
Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0782253676

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**DONGLONG INVESTMENT COMPANY LIMITED** anatangaza kupotelewa na kadi ya Pikipiki yenye namba za usajili **T 338 BLD – SHINERAY.** Chassis namba **LXYJCKL04A0344367**. Engine namba **162FMJAF063017**. Yeyote atakayaiona atoe taarifa kituo cha Polisi.

**Taarifa ya Polisi: DR/MAG/RB/825458/2020.**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA WILAYA MOROGRO**
**MAOMBI NA.78 MWAKA 2020.**
**TAUSI SAID KITAMBI...............MUOMBAJI**
**MOHAMED MAJUTO KATUNDU & KATUNDU TRADER.............MJIBU MAOMBI**
**WITO/KUITWA SHAURINI KWA MOHAMED MAJUTO KATUNDU & KATUNDU TRADER**

Fahamu kwmba shauri hili limepangwa kutajwa/kusikilizwa **tarehe 15 mwezi 12 mwaka 2020** saa **2:00 Asubuhi** mbele ya Mwenyekiti M.Khasim
Hivyo unaamriwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa.
Amri hii Imetolewa kwa mkono wangu na nakiri/Muhuri wa Baraza hii leo **tarehe 30 mwezi 11 mwaka 2020.**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA MWANZO – MKUYUNI MWANZA**
**MADAI TALAKA 77/2020**
**EDITHER PROSPER RWIKOZE .......... MDAI**
**MASATU JACOBO ............ MDAIWA**

**YAH: KUITWA SHAURINI**
Kwa kuwa mdai aliyetajwa hapo juu amefungua shauri dhidi yako kuhusiana na madai ya Talaka Unatakiwa kufika katika Mahakama hii mnamo tarehe 18/12/2020 saa 2:30 asubuhi kujibu madai yaliyotolewa dhidi yako.
KUMBUKA KUWA: Usipohudhuria siku hiyo shauri litasikilizwa na kuamuliwa bila wewe kuwepo. Imetolewa kwa mkono wangu na chapa ya Mahakama hii leo tarehe 03/12/2020.

**HAKIMU**
**MAHAKAMA YA MWANZO – MKUYUNI**
**MWANZA**

---

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**JOSEPHAT S.T GADIYE** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **SUZUKI ESCUDO** yenye namba za usajili **T.605 BPE** chesis namba **TD11W50468,** yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi
Polisi taarifa
**DAR/URA/RB/854125/2020**

116038602

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA BUKOBA-KAGERA**
**MAOMBI NA 315/2020**
**GODFREY SYRIVAN.......................MWOMBAJI**
**DHIDI YA**
**CHRISTOPHER VICENT.................MUJIBU MAOMBI**
**KWA: CHRISTOPHER VICENT**
**(POPOTE PALE ULIPO)**

Unaarifiwa kuwa kesi Na.315/2020 imepangwa kutajwa tarehe 11.01.2021 mbele ye Mwenyekiti wa Baraza E.Mogasa saa 2.00 asubuhi,mahali-Bukoba Mjini.
Hivyo unaamuriwa kuhudhuria wewe mwenyewe /mwakilishi wako mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa.Usipohudhuria Baraza litasikiliza shauri upande mmoja na hukumu kutolewa dhidi yako.
AMRI hii imetolewa kwa mkono wangu na MUHURI wa Baraza hili leo tarehe 30.11.2020

MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA BUKOBA

---

**IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF MOROGORO**
**DISTRICT AT MOROGORO**
**PROBATE AND ADMINISTRATION**
**CAUSE NO.....9.....OF 2020**

**In the matter of the Estate of the late...**
**EDITHA ELIETH MNYONE**
**BY 1...EDINA ELIETH MNYONE**
**2..................**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceeding if they think fit before the grant of probate (or letter of administration) is made to the above- named petitioner.

Objection to the grant should be filed on or before the 11 day of 01...2021
Dated at MOROGORO this.. 10...day of 12 ...2020

---

## KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**Baraka Silas Mwamwezi** Anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki **TVS STAR** Yenye nambali za usajili **MC387CJH.** Chasis Namba **MD625AF46K1G09922** Ingine namba DF4GK1904863 Yeyote atakaye iona atoe taarifa kituo chochote cha polisi, Taarifa Ya polisi **DR/KIG/RB/851647/2020**

116038501

---

**IN THE RESIDENT MAGISTRATE COURT OF MOSHI**
**AT MOSHI**
**DC CIVIL CASE NO.5 OF 2020**
**1) CLEMENCE MBOWE MENT..........................1ST PLAINTIFF**
**2) DIDAS PATRICE MUSHI................................2ND PLAINTIFF**
**3) PASTORY GABRIEL TIMIRA..........................3RD PLAINTIFF**
**VERSUS**
**1)JULIUS TARIMO...........................................1ST DEFENDANT**
**2)AMAN SEMBEKE ........................................2ND DEFENDANT**
**3)AUSTOCK ALPHONCE MUSHI.......................3RD DEFENDANT**

**NOTICE OF MENTION/HEARING**

**TO: DEFENDANT.**
Take Notice that the above case has been fixed for mention in the Resident Magistrates Court of Moshi on 17th the day of December 2020.
You are hereby ordered to appear in person or by advocate of agent dully authorized to do so and you are directed to produce on that day any document under which you intend to rely in support of your case.
**TAKE FURTHER NOTICE** that, default of your appearance on that day afore mentioned the court will proceed with the matter in your absence.

Given under my hand and seal of this Court this 8th day of December, 2020

RESIDENT MAGISTRATE
MOSHI

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA HAKIMU MKAZI MWANZA MWANZA**
**SHAURI LA MADAI N A. 78 YA 2020**
**QUALITY MOTOR'S LTD MWANZA**
**DHIDI YA**
**AFRICAN WHEEL AND TYRES LTD MWANZA**
**KWA: AFRICAN WHEEL AND TYRES LTD MWANZA**

**KUITWA SHAURINI**
Napenda kukufahamisha kwamba shauri husika limepangwa tarehe 17/12/2020 katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Mwanza; Hivyo unatakiwa kufika Mahakamani bila kukosa au kutuma mwakilishi wako/wakili. Kutofika kwako/mwakilishi kutafaya shauri hili kusikilizwa na kutolewa uamuzi.
Imetolewa kwa amri ya Mahakama na kupigwa Muhuri leo hii tarehe 08/12/2020.

HAKIMU MKAZI
MWANZA

---

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**SINAMENGI KATOLELA MAHENGE** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **ISUZU** yenye namba za usajili **T 893 BPD.** Chassis namba **634596** Engine namba **81274.**Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilicho karibu.Taarifa ya polisi **DSM/PHQ/RB/853727/2020**

---

OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI
INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042,
DAR ES SALAAM.
MOB:
+255 - 0782253676

## NAMPULA AUCTION MART AND COMPANY LTD
### TANGAZO LA MNADA WA HADHARA WA MARUDIO

Kwa idhini tuliyopewa na mteja wetu **BANK OF AFRICA (BOA)** tutauza kwa njia ya mnada wa hadhara dhamana ya mdaiwa wao,ambayo ni nyumba iliyopo sinza. Mnada utafanyika mahari nyumba ilipo tarehe 20/12/2020

| JINA LA MDAIWA | DHAMANA | MAELEZO YA DHAMANA | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|
| ISSA MASOUD IDD | NYUMBA | CT NO 19492 PLOT N0 336 BLOCK'C' SINZA AREA ,L.O.NO 35471 | 20/12/2020 |

**MASHARTI YA MNADA:**
(a) atahazimika kulipa 25%ya bei iliyofikiwa katika mnada papo hapo asilimia iliyobakia .75%italipwa ndani ya siku 14 toka tarehe ya mnada huo.
(b) endapo mnunuzi atashidwa kulipa asilimia 25% siku ya mnada basi mshindi wa pili ana haki ya kuweka hela siku hiyohiyo .
(C) mnunuzi akishidwa kutimiza sharti la 75% malipo ya awali hayatarejeshwa na mnada utarudiwa
(d) Gharama za kubadilisha umiliki,kumtoa mtu kwenye nyumba na gharama nyingine zozote zitakazo jitokeza itakuwa juu ya mnunuzi .gharama zozote zitakazo jitokeza nje ya utaratibu wa kibenki natutahusika nazo

**MAWASILIANO** KWA MAELEZO ZAIDI WASILIANA NA DALALI WA BENKI MOBILE: 0782757829,0712050414/0719441711

## NOTISI/TANGAZO LA MNADA WA HADHARA
### MAS & ASSOCIATES CO. LIMITED & COURT BROKER

KWA IDHINI TULIYOPEWA NA NATIONAL BANK OF COMMERCE TANZANIA (NBC) TUTAUZA NYUMBA NA VIWANJA KWA NJIA YA MNADA WA HADHARA ILI KUFIDIA MADENI YOTE YANAYODAIWA NA NATIONAL BANK OF COMMERCE TANZANIA (NBC).

| NO | JINA LA AKAUNTI | MMILIKI WA DHAMANA | MALI ZILIZOWEKWA DHAMANA | MAHALI | MUDA |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | MIEMBE SABA OIL COMPANY LIMITED | MIEMBE SABA OIL COMPANY LIMITED | CTNO 83285 PLOT NO 76 | VISIGA KIBAHA | KUANZIA SAA NNE KAMILI ASUBUHI (04:00) |
| 2 | NICHOLAS ATANAS TILLYA | NICHOLAS ATANAS TILLYA | CT NO 107893 PLOT NO 35 AND 37/1 BLOCK U | CHANG'OMBE | KUANZIA SAA NNE KAMILI ASUBUHI (04:00) |
| 3 | NICHOLAS ATANAS TILLYA | NICHOLAS ATANAS TILLYA | NICHOLAS ATANAS TILLYA | TEMEKE | KUANZIA SAA NNE KAMILI ASUBUHI (04:00) |

**MASHARTI YA MNADA:**
- UKAGUZI UNAANZA MARA BAADA YA TANGAZO HILI, MASHARTI YA MNADA:
- MNUNUZI ANATAKIWA KULIPIA ASILIMIA 25% SIKU YA MNADA NA ASILIMIA 75% SIKU KUMI NA NNE (14) TOKA SIKU YA MNADA NA HUKIKOSA KULIPA MNADA UTARUDIWA NA FEDHA ULIZOLIPA HAZITARUDISHWA.
- GHARAMA ZA KUBADILISHA JINA ZA MALI NI ZA MNUNUZI MWENYEWE
- MTEJA ATATAKIWA KULIPA FEDHA TASLIM SIO HUNDI.

**MAWASILIANO** MAS & ASSOCIATES COMPANY LIMITED & COURT BROKER SIMU: 0712 667989 WOTE/ MNAKARIBISWA

UZA,
CHENYE THAMANI KUBWA KWA KUTANGAZA NASI KWA BEI POA
TUPIGIE 0782253676

OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com

VICTORIA FINANCE PLC
S.L.P 12102
Tel: +255 22 180328/2180510
MAKUMBUSHO DAR ES SALAAM

## TANGAZO LA MINADA YA HADHARA

**VICTORIA FINANCE PLC** INAPENDA KUUTANGAZIA UMMA WA WATANZANIA YA KWAMBA KWA IDHINI ITAKAYOTOA KWA KAMPUNI TOFAUTI ZA UDALALI INATARAJIA KUUZA KWA MNADA WA HADHARA DHAMANA ZA WADAIWA SUGU KAMA IFUATAVYO;

| NA | JINA LA MDAIWA | DHAMANA | AINA YA DHAMANA | DALALI | TAREHE |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | GODFREY E. KILENGA | GARI | TOYOTA MARK II T 960 DQL | J&J RECOVERIES | 19-12-2020 |
| 2 | ERICK MUKANDARA | GARI | VOLKSWAGEN TOURAGE T.598 BHX | J&J RECOVERIES | 19-12-2020 |

Minada yote itafanyika mahali husika katika muda na siku ambayo itatangazwa kupitia katika vipeperushi na magari ya matangazo kutokana na idhini itayotoka kutoka katika ofisi za wakuu wa wilaya wanaohusika.

**MASHARTI YA MNADA;**
- Asilimia 25% ya bei iliyofikia italipwa papo hapo na asilimia 75% iliyosalia ilipwe ndani ya siku kumi na nne. (14). Kwa kushindwa kufanya hivyo itapelekea mnada kurudiwa tena na pesa zilizolipwa kutokurudishwa.
- Taratibu na gharama za kubadili hati miliki kadi ya gari ni juu ya mnunuzi.

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji
THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# HADITHI

ILISEMWA hapo zamani kuwa dunia inaharibiwa na vitu viwili tu. Mapenzi na mali. Vitu hivi vinaweza kumfanya binadamu aende popote, afanye chochote kile ili awenavyo, wengine wanakwenda mbali zaidi mpaka ikiwezekana hata kutoa uhai wa wenzao.

Shani, binti wa kitajiri anapitia kwenye mikasa mikubwa mizito ya kupotezwa kwa wazazi wake na kumsababishia ukiwa na mawazo tele. Wakati ikionekana binti huyo pekee kwa wazazi wake akielekea kurithi utajiri wa wazazi wake, kiu ya damu inaanza kuwaingia baadhi ya ndugu za wazazi wake ili apoteze maisha, wao waweze kumiliki mali hizo. Hapo ndipo uhai wa Shani unapokuwa matatani na patashika nguo kuchanika inapoanza. Fuatilia mkasa huu kuburudisha, kuelimisha na kusikitisha.

# Mauaji Harusini-**42**

**Mtunzi anapatikana (0716 350534)**

**Na Adam Fungamwango**




"WAMEWAAMBIA ni nani yupo nyuma ya huu mpango?"

"Jim ndiye aliyewatuma. Na bosi tulivyofuatilia, tumegundua kuwa Jim ni ndugu wa George na Paul ambao tuliwakamata hivi karibuni kwa kosa la kula njama ya kumuua Fikiri kwa sumu."

"Basi kazi nzuri. Ila kuna nyongeza ya kazi hapa. Kwanza kabisa fanyeni kila njia, ili huyo jamaa Jim na ndugu yake Ben wakamatwe sawa?"

Amour aliitikia na kuagana na bosi wake. Eddy alirusha ngumi ya ushindi hewani. "Kazi inakaribia kwisha," alijisemea moyoni.

Kitendawili tayari kinaonekana kuwa kimeshaanza kuteguka. Alijua kuwa Jim na Ben ndiyo waliowatuma hawa jamaa kumuua Shani. Na hii ni baada ya ndugu zao kukamatwa. Na hata wao wenyewe wamejificha. Hawajulikani walipo kwani hata kwao hawaishi hapo kwa sasa.

Kingine, kwa namna ambayo hakutarajia tayari ameshapata mtu ambaye anahusika na mpango wa kumuua baba yake Shani, Patiyo mkewe Grace ambao walikuwa wametoka kufunga ndoa saa kadhaa tu zilizopita.

Kwa jinsi sakata zima alivyolifuatilia, aligundua kuwa inawezekana Jim akawa amewakodi watu walewale ambao walimuua mdogo wake Patiyo bila yeye kujua ili wamuue Shani.

Anachojua kuwa Jim na ndugu zake wanataka kumuua Shani kwa sababu ya uchu wa mali, lakini kitu ambacho kimekuwa bado kinamuumiza kichwa je, Patiyo na shangazi yake Grace waliuawa kwa sababu gani?

Akainua simu ya mkononi. "Amour, nimesahau kitu. Namhitaji Tamim Hussein kwenye eneo la tukio sawa?" Akakata simu baada ya kujibiwa.

Alijua kwa sababu Tamim anatajwa kuhusika na tukio hilo, basi ni yeye ndiye atakayekuwa anajua ni nani aliyewatuma kumuua Patiyo na mkewe na kwa sababu gani.

*****************************

Alikuwa mgumu kama jiwe. Hakutaka kuzungumza chochote. Licha ya kuwekwa kwenye kiti ambacho kinapitisha umeme, lakini Tamim Hussein alikuwa mgumu kuongea.

**Tayari kitu kilichopo mkononi mwake ni kuwa wauaji wa Patiyo na Grace na waliotaka kumuua Shani ni hao hao. Ila Jim, George, Ben na Paul siyo wao waliotaka kumuua ndugu yao kwa ajili ya mali.**

Eddy hakutaka kumtesa mtu mwingine yoyote kati ya wale waliokamatwa. Tayari wameshateswa na kutaja kuwa walitumwa na Jim.

Lakini kuna taarifa kuwa hawa ndiyo pia walitumiwa kumuua shangazi wake Grace na mumewe Patiyo.

Hili ndilo sasa lilikuwa kichwani mwake. Akipata ushahidi wa huu mchezo utakuwa umekwisha.

"Unasikia. Nguvu zitakuishia halafu utakufa bure. Mimi nina taarifa zako zote. Wewe ndiye uliyemuua Patiyo na mkewe Grace. Kwa mkono wako. Nina ushahidi na hilo. Ninachotaka wewe ukiri na useme tu ulikuwa na nani na ni nani aliwatuma," alisema Eddy na kumtazama kwa hasira Tamim.

"Kumbuka kitendo chochote cha kukana mzigo wote utakuelemea wewe." Alimtisha.

Eddy alikuwa na taarifa, lakini alikuwa hana ushahidi. Alichokuwa akikitaka hapo ni ushahidi tu ili hata kama wanakwenda mahakamani awe na ushahidi wa kutosha kumtia Tamim hatiani. Vinginevyo ni kazi bure.

Kwa mara ya kwanza uzalendo ukamshinda Tamim. Sasa alijua atakufa peke yake. Wale wote walioshirikiana nao watabaki salama.

Tamim alijua hapo ana kesi mbili. Ya kwanza ni ya kujaribu kumuua Shani. Hiyo yupo pamoja na wenzake kina Michael Sabuni, Tofiki Seif, Fadhili Kidaga na hata Jim na ndugu zake watatu.

Lakini kesi ya mauaji wenzake watakuwa hawapo, badala yake atabeba msalaba peke yake. Alijua kabisa kesi ya mauaji hukumu yake kama umehurumiwa sana ni kifungo cha maisha, vinginevyo ni kunyongwa hadi kufa.

Wakati huo alikuwa anamfikiria Abesh Abdallah. Huyu ndiye chanzo cha yote hayo. Huyu ndiye aliyewatuma kwenda kumuua Patiyo na mkewe. Na sababu kubwa ni mapenzi. Alikuwa anampenda mno Grace. Aliishi naye kwa muda mrefu, lakini hawakuweza kuoana kwa sababu mbalimbali. Kwanza kabisa ni tofauti za umani. Lakini pia Abesh alikuwa mwingi wa habari. Kumbe rafiki yake na tajiri mwenzake Patiyo alichukua fursa hiyo ya kutengena kumchukua na alipohakikisha kuwa hawapo pamoja, alimuona kabisa.

Hiyo ilimkera Abesh na kuamua kukodisha kikosi cha kina Tamim kwenda kumuua, muda mfupi tu baada ya kutoka kanisani. Hakutaka waishi hata kwa siku moja ndani ya ndoa.

Akinyongwa, Abesh ataishi kama mfalme. Hatokuwa tena na mtu wa kumuuliza wakati yeye ndiye chanzo cha yote.

Hilo lilimfanya Tamim aamue kuainisha ukweli wote ili kila mmoja abebe mzigo wake.

"Sikia, ukisema ukweli, kila mmoja atahukumiwa kutokana na kosa alilofanya tu. Hilo linaweza kusababisha ukapata hukumu ya kawaida tu, lakini ukijifanya kuficha, utaubeba msalaba wote wa mwenzako, utanyongwa tu." Eddy alizidi kumtisha.

"Basi nifungulie nitasema yote." Alisema kwa sauti ya kugugumia.

"Sema kwanza kama ni kweli au si kweli, halafu mengine tutajua baadaye."

"Ni kweli, mimi na wenzangu hawa hawa tuliotaka kumuua Shani ndiyo tuliomuua Patiyo na mkewe."

Hasira ilimjaa Eddy. Lakini aliizuia kwa sababu ya kazi yake, hakutakiwa kufanya hivyo.

"Nani aliyefyatua risasi kuwapiga?"

Tamim aliinamisha kichwa kama mtu anayefikiria.

"Hutaki kusema ee, tuwashe kitufe cha umeme tena?"

"Hapana ni mimi?"

"Kwa nini wewe?"

"Mimi ndiye mlenga shabaha, kila mtu alipewa jukumu lake."

"Kwa nini mlimuua Patiyo na mkewe?"

"Tulitumwa na kupewa pesa nzuri tu."

"Ni nani aliwatuma."

"Abesh Abdallah." Alijibu Tamim na kujiona ametua mzigo mzito uliokuwa unamwelemea.

Eddy aliduwaa. Hakutegemea kama Tamim atalitaja jina hilo.

Ni jina la mtu mzito. Mfanyabiashara mkubwa nchini anayefahamika hata na watoto wadogo.

Ni mfanyabiashara ambaye umaarufu wake mkubwa ni mabasi ya kusafiri mikoani.

Hii ilimfanya kwa mbali Eddy atetemeke.

Sababu iliyotajwa ya kimapenzi, ilimfanya Eddy kujua kuwa kumbe shangazi yake kabla ya kufunga ndoa ya Patiyo alikuwa ni mpenzi wa Abesh.

Kumbe ilikuwa ni kesi ya matajiri wawili waliochukuliana wapenzi.

Wakati Tamim alieleza, Eddy alikuwa akirekodi kwenye simu yake maalum ya mkononi kwa ajili ya ushahidi.

Tayari kitu kilichopo mkononi mwake ni kuwa wauaji wa Patiyo na Grace na waliotaka kumuua Shani ni hao hao. Ila Jim, George, Ben na Paul siyo wao waliotaka kumuua ndugu yao kwa ajili ya mali.

Grace na Patiyo waliuawa kwa ugomvi wa kimapenzi, lakini wao walitaka kumuua Shani kwa sababu ya kutaka kurithi mali ya kaka yao kwa sababu tu alikuwa na binti huyo tu pekee.

Mlango ulifunguka. Amour aliingia na wenzake watatu, walikuwa wameongozana na watu wengine wawili ambao Eddy hakuwafahamu.

"Bosi hawa wawili ni Jim na Ben ambao walikuwa wametoroka. Tumewakamata leo. Hawa wanatakiwa kuunganishwa kwenye kesi ya George na Paul ya kutaka kumuua Shani." Amour alimhabarisha.

**ITAENDELEA JUMAMOSI**

# RASHFORD: NITASTAAFU SOKA NIKIWA MAN UNITED




**MANCHESTER,** England

MARCUS Rashford amesema anahitaji kumaliza maisha yake ya soka la ushindani akiwa ndani ya Manchester United kwa sababu anaipenda.

Mshambuliaji huyo mwenye miaka 23 alikuwa anatajwa kuingia kwenye rada za Manchester City pamoja na Chelsea ambao walikuwa wanatajwa wanahitaji saini yake.

Rashford amekuwa ni mchezaji muhimu kwenye kikosi cha kwanza baada ya kupandishwa kutoka kwenye Akademi ya timu hiyo inayoshiriki Ligi Kuu England, ambapo kesho itakuwa na mchezo dhidi ya Manchester City kwenye Uwanja wa Old Trafford.

Ikiwa ipo nafasi ya sita na pointi zake 19 inakutana na City iliyo nafasi ya saba na pointi zake 18 jambo linalomaanisha kwamba mchezo huo utakuwa na ushindani mkubwa.

Rashford amesema:"Sijawahi kufikiria kuwa nje ya Old Trafford kwa kuwa nilikuwa ninafurahia maisha ya hapa tangu zama zile nikiwa mtoto, ninapenda maisha ya hapa nilipo.

"Kwenye akili zangu sijawahi kufikiria kuhusu siku moja kutoa uzi ambao ninao kwa sasa na kuvaa uzi mwingine, sijafikiria timu nyingine ya kwenda zaidi ya Manchester United.

"Nina matumaini ya kufanya vizuri zaidi hapa nilipo kwa sasa na hilo linawezekana kwa kuwa uwezo na nia ipo."

# Ronaldo aisikitikia Barcelona

**TURIN,** Italia

CRISTIANO Ronaldo amefunguka na kusema yeye si mpinzani wa Lionel Messi, lakini ni rafiki yake na wamekuwa na uhusiano mzuri, huku akiweka wazi kuwa anaona timu hiyo siku za hivi karibuni haifanyi vizuri.

Desemba 8, mwaka huu Ronaldo alikutana na Messi kwa mara nyingine kwenye Uwanja wa Camp Nou katika mchezo wa Ligi ya Mabingwa Ulaya kati ya Barcelona na Juventus.

Wenyeji Juventus waliibuka na ushindi wa mabao 3-0, huku mabao mawili yakifungwa na Ronaldo kwa njia ya penalti.


Ronaldo alirudi Hispania kwa mara ya kwanza hivi karibuni kucheza tangu aondoke Real Madrid, lakini amewahi kucheza dhidi ya Valencia na Atletico Madrid akiwa mchezaji wa Juventus.

"Tumekuwa na uhusiano mzuri kwa kipindi chote na Messi. Sioni kama ni mpinzani wangu. Kila mmoja wetu amekuwa katika ubora wake hasa akiwa na timu yake jambo ambalo ni zuri.

"Nimefurahia kurudi tena Hispania hasa hapa Katalunya. Imekuwa ngumu kucheza ndani ya Camp Nou tena dhidi ya timu bora ambayo imekuwa si rahisi kupambana nayo.

"Lakini tumecheza kama timu kwa hiyo sisi ni washindi na mabingwa wa familia moja kwani jinsi tulivyocheza hakuna cha kutukwamisha zaidi kuongeza bidii na kufika mbali.

"Kama unafunga mabao matatu hapa Camp Nou basi ni wazi unastahili kumaliza nafasi ya kwanza. Ingawa naona Barcelona kwa sasa haifanyi vizuri," amesema Ronaldo.






# *Sura ya Maradona kuwekwa kwenye fedha*

**BUENOS AIRES,** Argentina

NORMA Durango ambaye ni seneta wa Bunge la Argentina amewasilisha muswada bungeni akipendekeza picha ya gwiji wa soka duniani, Diego Maradona, aliyefariki Novemba 25, 2020 kuwekwa kwenye fedha.

Mbunge huyo amependekeza sura ya Maradona iwekwe kwenye noti ya peso 1,000 ambayo ni sawa na Sh. 27,600 za Tanzania.

Durango amesema lengo ni kumwenzi nyota huyo kwa heshima aliyolipa taifa hilo mwaka 1986 baada ya kuiwezesha Argentina kutwaa Kombe la Dunia na kuiandika historia ya nchi hiyo katika ramani ya soka duniani.

Noti hiyo itaonyesha sura ya Maradona huku upande mwingine ikionyesha goli maarufu alilofunga kwenye mchezo wa robo fainali dhidi ya England mwaka 1986.

Maradona ambaye amewahi kuchezea klabu kadhaa duniani ikiwamo Napoli ya Italia na FC Barcelona kabla ya kustaafu soka kufuatia kuathiriwa na matumizi ya dawa za kulevya, alifariki kwa mshtuko wa moyo.

# Haaland kuuzwa kwa euro milioni 75

**DORTMUND,** Ujerumani

ERLING Haaland ameripotiwa kwamba atakuwa tayari kuuzwa kwa euro milioni 75 mwakani, kwa mujibu wa ESPN.

Haaland amekuwa akihusishwa na mpango wa kuondoka pale Borussia Dortmund baada ya kuwa na kiwango cha kuvutia na miamba hao wa Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 20 anaweza kuwa sokoni mwakani na bei yake haitaweza kushuka.

Na Dortmund wameweka wazi kwamba, hawataweza kumwachia Haaland chini ya kiasi cha euro milioni 75.

Real Madrid imekuwa ikihusishwa zaidi na mpango wa kutaka kumsajili fowadi huyo, huku pia Manchester United na Liverpool zikionyesha nia ya kuhitaji saini yake.

Haaland, ambaye kwa sasa ni majeruhi, amefunga mabao 33 katika mechi 32 za mashindano yote tangu atue hapo kutoka Dortmund akitokea Salzburg, Januari, mwaka huu.





# MAN UNITED YAMJIBU WAKALA WA POGBA

**MANCHESTER,** England

KLABU ya Manchester United imemjibu wakala wa Paul Pogba na wamebainisha wanaweza kumuuza nyota huyo wakati wa dirisha dogo la Januari.

Mino Raiola alinukuliwa wiki iliyopita akisema Pogba hana furaha na maisha ya Old Trafford na kuwa muda wake umefika mwisho.

Wakala huyo alienda mbali zaidi kwa kusema Pogba mwenyewe yupo tayari kuondoka wakati wowote na hivyo kwa sasa ni suala la muda tu.

Kwa mujibu wa gazeti la Daily Mail, limemnukuu mmoja wa vigogo wa Manchester United akisema kwamba, wao hawana mpango wa kuendelea kubakia na Pogba.

Kwa mujibu wa ripoti hiyo, kigogo huyo amesema tayari mipango inaendelea kuhakikisha wanamuuza haraka inavyowezekana.

Pogba amekuwa akihusishwa na mpango wa kurejea katika klabu yake ya zamani ya Juventus.

Lakini pia, Real Madrid inayonolewa na Mfaransa mwenzake, Zinedine Zidane imekuwa ikimnyatia nyota huyo.

Mkataba wa sasa wa Pogba unatarajiwa kumalizika mwaka 2022.

# *Kocha amsifia Hauge*

**MILAN,** Italia

KOCHA Mkuu wa AC Milan, Stefano Pioli amemsifia Jens Petter Hauge baada ya kuonyesha kiwango kizuri wakati wa mchezo wao wa ushindi dhidi ya Sparta Prague kwenye Ligi ya Europa, juzi Alhamisi.

Bao la Hauge la kipindi cha kwanza, lilishuhudia Milan ikiibuka na ushindi wa 1-0 dhidi ya Sparta 1-0 na kuwafanya Rossoneri hao kukaa kileleni mwa kundi H.

Nyota huyo mwenye umri wa miaka 21 alicheza vizuri na Tomas Wiesner kabla ya kutupia bao hilo nyavuni na golikipa, Milan Heca kushindwa kudaka.

Hauge ni mchezaji mwenye umri mdogo zaidi kwenye Ligi Kuu Italia, Serie A, akiwa na mabao manne kwenye mashindano yote msimu huu.

Amefunga mabao manne kwenye mashindano yote kwa msimu huu wa 2020-21 amefunga mabao manne tangu kuwasili kutoka klabu ya Norway ya Bodo/Glimt mwanzoni mwa msimu huu na Pioli alimsifia.

"Ni mchezaji aliyekamilika, na anaweza kubadilisha matokeo wakati wowote," alisema Pioli akiiambia Sky Sport Italia.



# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# NAWEZA KUMBAKIZA MESSI BARCA – FONT

**Mgombea urais ajinadi anaweza kumbakisha nyota huyo ambaye anawindwa na klabu...**

**BARCELONA,** Hispania

MGOMBEA wa urais wa Barcelona, Victor Font, anaamini anaweza kumshawishi nyota, Lionel Messi kubakia pale Camp Nou baada ya msimu huu.

**Majaliwa ya Messi yamekuwa mjadala muhimu kwa miamba hao wa Ligi Kuu Hispania, LaLiga, baada ya nyota huyo kuwasilisha maombi ya kutaka kuondoka baada ya kuwa na msimu mbaya wa 2019-20.**

Mshindi huyo mara sita wa Ballon d'Or alikuwa akihusishwa na mpango wa kujiunga na miamba wa Ligi Kuu England, Manchester City kabla ya kuamua kubakia nchini Hispania, ingawa pia amekuwa akihusishwa na mabingwa wa Ligi Kuu Ufaransa, Ligue 1, Paris Saint-Germain na Inter Milan.

Font, ambaye anawania nafasi ya urais katika uchaguzi utakaofanyika Januari 24, mwakani baada ya kujiuzulu kwa Josep Maria Bartomeu Oktoba, mwaka huu, amezungumzia umuhimu wa kumbakisha Messi.

"Nashawishika kwamba yeye ni mshindani na anataka timu ya ushindi na kwa uhakika kabisa nitambakisha Messi ili aweze kustaafu soka hapa," alisema Font akinukuliwa na ESPN.

"Messi ni mchezaji bora kwenye historia ya mchezo namba moja duniani wa soka. Fikiria hilo linamaanisha nini.

"Kwa sababu hiyo, uwezo wa Messi hapa Barca ni jambo muhimu zaidi kwa kikosi chetu na nitafanya kila niwezalo kuhakikisha anabakia hapa baada ya msimu huu.

"Kumbakisha yeye wakati wa dirisha kubwa la usajili wa kipindi cha majira ya joto ndio jambo muhimu zaidi kwa sasa.

"Messi anatakiwa kuendelea kuwa kwenye klabu hii kwa namna yoyote ile, hivyo nina imani ninao uwezo wa kufanya hivyo."

Messi amefunga mabao manne kwenye mechi 10 za LaLiga msimu huu, huku mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 33 amefunga mabao saba katika mashindano yote.

## ZISIKUPITE

### UNITED YAMTAKA WHITE

MANCHESTER United imemwongeza mlinzi wa Brighton, Ben White kwenye orodha ya wachezaji inaowataka. Anajumuishwa na wachezaji wengine ambao ni Dayot Upamecano mwenye umri wa miaka 22 kutoka RB Leipzig na Raphael Verane wa Real Madrid (27). ***(MEN)***

### ALLI AKARIBIA PSG

KLABU ya Paris St-Germain wanajiandaa kufanya uhamisho wa mkopo ifikapo Januari, mwakani kwa kiungo wa kati wa Tottenham, Dele Alli na inaamini Spurs wamejiandaa kumwachia mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24. ***(Mail)***

### ALABA KUIKAMUA CHELSEA

CHELSEA itahitaji kumfanya David Alaba kuwa mchezaji wao anayelipwa kitita kikubwa zaidi kama watatakiwa kumchukua ili atue Stamford Bridge kutoka kule Bayern Munich.***(Mirror)***

### ARTETA AMTAKA GRACIA

KOCHA wa Arsenal, Mikel Arteta ana mpango wa kumsajili mlinzi wa Hispania, Eric Garcia mwenye umri wa miaka 19 kutoka klabu yake ya zamani ya Manchester City. ***(Sun)***

### ROJO ANUKIA SHEFFIELD

KLABU ya Sheffield United wanafikiria kumnyakua mlinzi wa Manchester United, Marcos Rojo, 30. ***(Mail)***

### ERIKSEN MAMBO MAGUMU

MSHAHARA wa kiungo wa kati wa Denmark, Christian Eriksen kule Inter Milan huenda ukamfanya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28 kupunguzwa katika kikosi hicho ili arudi kwenye Ligi Kuu England. ***(Telegraph - subscription required)***

### SZOBOSZLAI NJIA NYEUPE

KUSHINDWA kusonga mbele kwa Red Bull Salzburg kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, kumeongeza matumaini ya Arsenal kumsajili kiungo wake wa kati, Dominik Szoboszlai ifikapo Januari. ***(Football London)***

### FOLARIN KUBAKI ARSENAL

KOCHA wa Arsenal, Mikel Arteta ana matumaini ya kuendelea kumbakisha, Folarin Balogun katika klabu hiyo. Mkataba wa mshambuliaji huyo utamalizika msimu ujao. ***(Metro)***

### BILIC AKALIA KUTI KAVU

KLABU ya West Brom imeanza kubainisha mbadala wa kocha, Slaven Bilic, ambaye huenda akapoteza ajira yake ikiwa kikosi chake kitapigwa na Newcastle leo Jumamosi. ***(Mail)***

### BAYERN YAMKATAA HAALAND

MKURUGENZI Mtendaji wa Bayern Munich, Karl-Heinz Rummenigge amesema mabingwa hao wa Ujerumani hawahitaji kumsajili mshambuliaji wa Norway, Erling Braut Halaand (20), kwa sababu wana mshambuliaji wa Poland, Robert Lewandowski ambaye ana umri wa miaka 32. ***(Tuttosport)***

## HABARI MICHEZO

## Wakala ambakisha Kagere Msimbazi

**Na Shufaa Lyimo**

WAKALA na Meneja wa mshambuliaji wa Simba, Meddie Kagere, Patrick Gakumba amezitolea nje timu ambazo zinahitaji kumsajili mchezaji huyo katika kipindi cha dirisha dogo ambalo litafunguliwa kuanzia Desemba 15, mwaka huu.

Akizungumza jana na gazeti hili jana, Gakumba alisema amepokea maombi kutoka katika timu mbalimbali zinazoshiriki Ligi Kuu Bara na nje ya Tanzania zikionyesha nia ya kupata huduma ya Kagere.

Gakumba alisema amekataa kutoa baraka za kumsajili Mnyarwanda huyo kwa sababu bado ni mchezaji halali wa Simba.

"Nimepokea maombi mengi kutoka kwenye klabu mbalimbali ambazo siwezi kuzitaja zikiomba kumsajili Kagere katika usajili wa dirisha dogo, zikidai sasa hivi hapangwi mara kwa mara, lakini nimewakatalia kwa sababu najua bado ni mchezaji halali wa Simba," alisema Gakumba.

Wakala huyo alisema Kagere ni mchezaji mzuri ambaye anategemewa ndani ya kikosi cha Simba ambacho kinahitaji kutaka kuwa na mchezaji mwenye uwezo mzuri.

Aliongeza amekuwa akiiombea Simba mafanikio katika mechi zake za kimataifa pamoja na Ligi Kuu Tanzania Bara.

## Mkwasa afunguka kilichombeba Bara

**Na Sabato Kasika**

NYOTA wa muziki wa kizazi kipya, mwanadada Pamela Daffa (Pam D), ambaye sasa anatamba na wimbo mpya wa 'Mambeza', amesema anajiandaa kutambulisha video wiki ijayo.

Akizungumza na gazeti hili, msanii huyo anasema alipanga kutambulisha video hiyo mwezi uliopita, lakini akashas (kizazi kipya) na Christian Bella anayetamba katika muziki wa dansi.

"Ninafanya hivyo ili mashabiki waone kuna utofauti wa vionjo katika nyimbo, sio kwamba ninataka kubebwa...huo ni ubunifu wangu nilioamua kuufanya ili kutoa burudani ya ladha tofauti," amesema.

Pam D, ametaja wimbo ambao amemshirikisha Bella kuwa ni 'Ngoma Droo' na kufafanua kuwa hadi sasa unaendelea kutamba licha ya kuwapo wimbo mpya wa 'Mambeza' aliofyatua hivi karibuni

"Baadhi ya maneno yaliyomo katika wimbo wa 'Mambeza ni Umbea ulianza zamani tangu ningali mdogo, sasa nimekuwa nami nawasema wambeya', video yake ilishakamilika," amesema.

Nyota huyo wakati anaanza muziki, amewahi kutamba na nyimbo za 'Nimempata', 'Popo Lipopo' na 'Nipe Nono', ambazo zilitayarishwa na Mesen Selekta, na kumwezesha kuwa miongoni mwa wasanii maarufu.

# YANGA PRINCESS YATAMBA KUICHAPA SIMBA QUEENS

**Na Adam Fungamwango**

MABINGWA watetezi wa Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania (SWPL), Simba Queens wanatarajia kuwakaribisha watani zao Yanga Princess katika mechi ya mzunguko wa kwanza itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Mo Arena, Bunju jijini, Dar es Salaam.

**Kocha Mkuu wa Yanga Princess, Edna Lema, alisema kikosi chake kiko imara na kimejiandaa kupata matokeo mazuri katika mchezo huo.**

Lema alisema wachezaji wake wote wako fiti na anaamini watafanikiwa kuondoka na ushindi ili kuendelea kukaa kileleni katika msimamo wa ligi hiyo.

Naye Kocha Mkuu wa Simba Queens, Mussa Hassan 'Mgosi', aliliambia gazeti hili mechi hiyo haitakuwa rahisi kwa sababu Yanga Princess wamejipanga vizuri msimu huu na pia wanataka kulipiza kisasi cha kufungwa kila wanapokutana.

"Watakachofanya sana ni kupunguza idadi ya magoli ambayo huwa tunawafunga, tunajua Yanga Princess wanaongoza ligi, lakini tuliangalia na kufanya tathmini tukaona timu ambazo wamecheza nazo ni zile ambazo hazijiwezi sana na sisi tumecheza na timu ngumu, kwa hiyo tunataka tupate ushindi kwao ili tusonge huko juu," alisema Mgosi.

Alisema wataingia kuikabili Yanga Princess kwa tahadhari kubwa, lengo ni kukwea kileleni kwenye msimamo wa ligi na anatambua dhamira ya wapinzani wao.

Tangu Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania ilipoanzishwa, Simba Queens imekuwa ikiibugiza mabao Yanga Princess.

Desemba mwaka jana, Yanga ilichapwa mabao 3-1 kwenye mechi ya misimu miwili iliyopita na Januari, mwaka huu ilikubali kichapo kingine cha magoli 7-0, kabla ya kuchapwa mabao 5-1 Juni, mwaka huu.

Yanga Princess inaongoza ligi ikiwa na pointi tisa, ikishinda mechi zote tatu sawa na Alliance Girls, wakati Simba Queens yenye pointi saba iko kwenye nafasi ya tatu.




Mshindi wa bonasi ya Jackpot wa wiki iliyopita, Juma Chilowe (23), akiwa na hundi yake ya mfano ya Sh. milioni 21.9 baada ya kubashiri kwa usahihi mechi 12 kati ya 13 kwenye Jackpot ya SportPesa. Jackpot ya wiki hii ni Sh. milioni 331.2. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# JKT Tanzania yaiita Yanga SC

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa klabu ya JKT Tanzania inayoshiriki Ligi Kuu Bara, umesema milango iko wazi kwa klabu yoyote inayohitaji huduma ya mshambuliaji wake, Adam Adam, imefahamika.

Akizungumza na gazeti hili jana, Katibu Mkuu wa JKT Tanzania, Abdul Nyumba, alisema klabu yake haijapokea barua rasmi ya kutakiwa kwa mshambuliaji huyo ambaye bado ana mkataba na maafande hao.

Nyumba alisema itakuwa tayari kufanya mazungumzo na klabu itakayofuata taratibu na sheria za usajili kwa ajili ya kumnunua mshambuliaji huyo ambaye mapema mwaka huu alisaini mkataba wa mwaka mmoja na nusu.

"Soka ni ajira kubwa, kama Yanga itakapokuja na kufuata utaratibu wa soka na masharti ya mkataba wetu hatutakuwa na hiyana ya kumzuia mchezaji huyo kwenda katika timu hiyo inayomuhitaji."

"Masharti yaliyoko katika mkataba wetu yana vipengele vitatu, maridhiano kati ya mchezaji na klabu (maslahi ya kifedha), pande zote tatu, klabu inatakiwa kununua sehemu ya mkataba uliobakia na mwisho kutakiwa kulipa fedha kama kutakuwa na ada ya usajili," alisema Nyumba.

Adam ni miongoni mwa wachezaji ambao wanatajwa kuwindwa na Yanga katika usajili wa dirisha dogo litakalofunguliwa ifikapo Desemba 15, mwaka huu.

Nyota huyo yuko katika nafasi ya pili kwenye orodha ya wafungaji wa Ligi Kuu Bara akiwa na mabao sita wakati kinara ni nahodha wa mabingwa watetezi, Simba, John Bocco.

# Michezo

Jumamosi Desemba 12, 2020

Nipashe




Sura ya Maradona kuwekwa kwenye fedha UKURASA 20



Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Simba, Haji Manara (kushoto), akiwa na mkewe, Naheeda Abdallah, baada ya kufunga ndoa katika msikiti wa Al Maamur ulioko Upanga jijini, Dar es Salaam juzi. Sherehe rasmi ya wanandoa hao itafanyika leo usiku. **PICHA: MTANDAO**

## Simba yahamishia 'mafuriko' Sokoine

**Na Mwandishi Wetu**

KIKOSI cha mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba kilitua salama Mbeya tayari kuwavaa wenyeji Mbeya City katika mchezo wa ligi hiyo utakaochezwa kesho kwenye Uwanja wa Kumbukumbu ya Sokoine jijini humo.

Simba itashuka katika mchezo leo ikiwa na kumbukumbu ya ushindi wa mabao 2-0 walioupata dhidi ya Polisi Tanzania wakati wenyeji wao wamekuwa na matokeo ya kusuasua tangu kuanza kwa msimu huu wa 2020/21.

Kocha Mkuu wa Simba, Sven Vandenbroeck aliliambia gazeti hili kikosi chake kinahitaji ushindi tu ili kiendelee kujiweka katika mazingira bora ya kutetea taji la ligi hiyo wanalishikilia.

Sve alisema wamejipanga kuwaheshimu wapinzani wao na watawakabili bila ya kuangalia matokeo ya mechi walizofanya vibaya.

"Tunataka pointi tatu kwenye kila mechi, tukifanikiwa kushindwa mechi zote tutawakaribia wapinzani, bado safari ni ngumu na kila mmoja hataki kukaa nje ya mstari," Sven alisema.

Mbeya City yenye pointi 12, imecheza mechi 14 na kati ya hizo imeshinda michezo miwili, huku imetoka sare mara sita sawa na idadi iliyopoteza, ikiwa kwenye nafasi ya 15 wakati Yanga yenye pointi 34, ndio vinara wakifuatiwa na Azam FC yenye alama 27.

Msimu uliopita mchezo wa mzunguko wa pili uliochezwa Uwanja wa Sokoine, Simba ilishinda mabao 2-0.

Baada ya mechi hiyo, Simba itarejea jijini Dar es Salaam tayari kwa mchezo wake mwingine wa kiporo dhidi ya KMC FC utakaochezwa Desemba 16, mwaka huu kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa.

# Yanga: Mwadui hawachomoki

### ●●● Hata hivyo wenyeji wawataka vinara hao kukumbuka kilichowakuta watani zao...

**Na Saada Akida**

POINTI tatu ndio neno pekee linalotajwa na Kocha Mkuu wa Yanga, Cedric Kaze, kuelekea mchezo wao wa Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Mwadui FC utakaochezwa leo kwenye Uwanja wa Kumbukumbu ya Kambarage mkoani Shinyanga.

**Akizungumza na gazeti hili jana, Kaze alisema wachezaji wake wote walioko kwenye safari ya Shinyanga wapo fiti na wana ari ya kutafuta matokeo chanya katika mchezo huo.**

Kaze alisema anatarajia mchezo huo utakuwa na ushindani kwa sababu timu zote zimejiandaa kutafuta ushindi licha ya kuwa na rekodi tofauti, wenyeji wakidhamiria 'kuzinduka'.

Kocha huyo alisema ana imani na wachezaji wake wataongeza umakini na kucheza kwa juhudi kama walivyoshuka dimbani kwenye michezo iliyopita.

"Malengo yetu ni kuingia uwanjani kutafuta pointi tatu muhimu katika kila mechi, Mwadui FC sio ya kuibeza, haikuwa na matokeo mazuri katika michezo ya nyuma, na kwa kuzingatia hilo, mechi ya kesho (leo), itakuwa na ushindani mkubwa, tumejiandaa kukabiliana na hali hiyo, hata hivyo dhamira yetu ni kushinda na si jambo lingine," alisema Kaze.

Alieleza Ligi Kuu Tanzania Bara ni ngumu na hasa wanapocheza na timu za nje ya Dar es Salaam kwa sababu zimejipanga kutumia vyema viwanja vyao vya nyumbani.

Naye Kocha Mkuu wa Mwadui FC, Adam Khalid, alisema msimu huu hawakuanza vizuri, lakini tayari wameshakaa na kubaini walipokosea.

Khalid alisema kwa sasa vijana wake wako imara na kamili kuwakabili Yanga huku wakijiandaa 'kuvunja mwiko' wa Yanga ambayo haijapoteza mechi hata moja msimu huu.

"Wachezaji wangu wote wako fiti, tunawaheshimu Yanga, tutacheza kwa tahadhari kubwa kwa sababu tunahitaji kuvunja mwiko wa Yanga, sisi tuwe timu ya kwanza kuwafunga kama ilivyokuwa kwa msimu uliopita tulipokutana na Simba."

"Turudi msimu uliopita Simba ilikuja kucheza na sisi ikiwa haijapoteza mechi ila kwetu walishindwa kufurukuta, sasa Yanga wanahitaji kuja kwa tahadhari kwa sababu msimu huu 'dozi' imedondokea kwao," alisema kocha huyo.

Aliongeza hana mchezaji ambaye ni majeruhi, hivyo ana uhuru wa kupanga 'kikosi kazi' kitakachopambana kusaka matokeo mazuri.

"Sisi tunazihitaji zaidi pointi kuliko Yanga, tulianza vibaya msimu, lakini tumejiuliza na kupata jibu tulipokosea, tutarejea kwenye ushindani kuanzia mechi hii dhidi ya Yanga, inawezekana kama tutatekeleza mipango tuliyoiandaa," aliongeza kocha huyo.

Yanga itashuka tena dimbani bila ya huduma ya kiungo wake wa kimataifa kutoka Angola, Carlos Carlinhos ambaye anasumbuliwa na maumivu ya nyonga.

Katika msimamo wa ligi, Yanga yenye pointi 34 ndio vinara wa ligi hiyo wakati Mwadui FC wakiwa katika nafasi ya 17 wana pointi pointi 10, timu zote zimecheza michezo 14.


9 770856 541002 >

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042